
**haribika** to be ruined or spoiled.
*Baiskeli yangu imeharibika; haiwezi kwenda.*

**haribu** to ruin or spoil something.
*Watoto walicheza na tochi yangu, wakaiharibu.*

**harufu** (harufu) a smell.
*Nasikia harufu mbaya.*

**harusi** (harusi) (or arusi) a wedding—that is, the ceremony when two people marry each other.
*Siku ya harusi ni siku ya furaha.*

**hasa** exactly; just right; very much.
*Hesabu vitu hivi hasa.*

*Nampenda hasa huyu.*

**hasara** (hasara) loss, such as the money which a trader loses if he sells something for not as much as it cost, or if he cannot sell something at all.
*Mwuzaji alipata hasara kubwa wakati duka lake lilipochomeka moto.*

**hasira** (hasira) anger; being angry.
*Mwalimu anaonyesha hasira nyingi. Mimi sina hasira.*

**hata** even.
*Hata nitamfukuza. Simpendi hata kidogo.*

**hatari** (hatari) danger; something dangerous; being dangerous.
*Moto ni hatari sana.*

**hatua** (hatua) a step.
*Nenda mbele, hatua tatu.*

**hatujambo** we are fine, thank you.
*Hatujambo sana.*

**hawa** these; these ones.
*Hawa ni wazazi.*
*Sitawasaidia hawa.*

**haya** these; these ones.
*Haya ni mawe. Tupa haya yote.*

**haya** (haya) modesty; being not proud or not bold.
*Mtoto huyu anaonyesha haya.*

**hayo** those; those ones; those ones we have been talking about; those ones over there near you.
*Nataka matunda hayo.*

**hebu** I say!
*Hebu, nipe kalamu yangu.*

**hekima** (hekima) wisdom—that is, what a wise man knows.
*Watu wazima huwa na hekima kuliko watoto.*

**hela** (hela) a coin; money.
*Nimepoteza hela yangu.*

**hema** (hema) a tent—that is, a kind of house made of thick cloth.
*Tulipofika kiwanjani tulisimamisha hema zetu.*

**hesabu** to count.
*Hesabu moja mpaka kumi.*

**hesabu** (hesabu) a counting; arithmetic; studying numbers.
*Napenda kusoma kitabu changu cha hesabu.*

**heshima** (heshima) respect; behaving well towards someone or something.
*Rais wa nchi astahili heshima.*

**heshimu** to respect—that is, to behave nicely toward someone who is worthy of it.
*Lazima mtoto amheshimu mzee.*

**hewa** (hewa) air.
*Kwenye mwezi hakuna hewa yo yote.*

**hiari** (hiari) a choice; what someone chooses.
*Sina hiari ila kulipa madeni yangu. Alifanya hivyo kwa hiari yake.*

**hicho** that; that one; that one we have been talking about; that one over there near you.
*Hicho ni kitabu chako.*

**hifadhi** to keep something safe.
*Serikali inatutaka kuhifadhi wanyama kama vifaru.*

**hii** this; this one; these; these ones.
*Sitaki kalamu hii. Hii ni miti michanga.*

**hiki** this; this one.
*Hiki ni kitabu. Nataka hiki.*

**hila** (hila) a trick, especially a clever, bad trick.
*Amesema uwongo kwa hila fulani.*

**hili** this; this one.
*Hili ni ua zuri. Chuma hili.*

**hilo** that; that one; that one we have been talking about; that one over there near you.
*Nipe papai hilo.*

**himiza** to make something or someone go quickly.
*Nilimhimiza Hamisi asichelewe.*

**historia** (historia) history.
*Vitabu vya historia vyatufundisha mambo ya zamani.*
**hitaji** to need.
*Anasikia kiu; anahitaji maji.*
**hitimu** to finish, especially to finish an education.
*Alipohitimu mafundisho, alianza kufanya kazi mjini Nairobi.*
**hivi** these; these ones.
*Hivi ni viatu. Napenda hivi.*
**hivi** this way.
*Fanya hivi.*
**hivyo** those; those ones; those ones we have been talking about; those ones over there near you.
*Hivyo ni viatu vyako.*
**hivyo** that way.
*Usifanye hivyo!*
**hiyo** that; that one; that one we have been talking about; that one over there near you.
*Hiyo ni kalamu yako.*
**hiyo** those; those ones; those ones we have been talking about; those ones over there near you.
*Mimea hiyo imemea vizuri sana.*
**hizi** these; these ones.
*Hizi ni karatasi. Chukua hizi.*
**hizo** those; those ones; those ones we have been talking about; those ones over there near you.
*Sitaki kalamu hizo.*
**hodari** very good at doing something; clever at doing something.
*Paulo ni mchezaji hodari. Watu hawa ni hodari katika kufanya kazi zao.*
**hodi** may I come in?
*Alisema, 'Hodi?' Nikasema, 'Karibu.'*
**hofu** (hofu) fear; being afraid.
*Alipomwona simba, alishikwa na hofu nyingi.*
**homa** (homa) a fever.
*Anna ameshikwa na homa mbaya sana.*
**honi** (honi) a horn.
*Dreva alipiga honi ya motokaa.*
**hospitali** (hospitali) a hospital.
*Hospitali hii ina vitanda arobaini.*
**hotuba** (hotuba) a speech—that is, what someone says when he speaks to a lot of people.
*Kwanza Bwana D.C. alitoa hotuba yake.*
**hudhuria** to attend—that is, to be one of a group of people meeting together.
*Watu wengi sana walihudhuria mkutano huo.*
**huenda** perhaps.
*Huenda ikapotea. Huenda Anna akachelewa.*
**hujambo** hello, how are you?
*Hujambo Bwana Ali?*
**huko** there.
*Utakwenda huko?*
**huku** while.
*Sitaki kumsumbua huku anafanya kazi. Alikimbia huku akilia.*
**huku** around here.
*Huku kuna waduduu wengi.*
**humo** in there.
*Aliingia humo shimoni.*
**humu** in here.
*Humu pangoni mna giza tele.*
**huo** that; that one; that one we have been talking about; that one over there near you.
*Huo ni mfuko wako. Utafanya nini na ufito huo?*
**huru** free.
*Wananchi wa Kenya ni watu huru. Sisi twajivunia Kenya Huru.*
**huruma** (huruma) sympathy or pity.
*Daktari alimtazama mgonjwa kwa huruma.*

**husu** having to do with someone or something.
*Jambo hili linanihusu mimi.*
**hutubia** to speak to a group of people.
*Rais aliwahutubia wananchi.*
**huu** this; this one.
*Huu ni ubao. Huu ni mfuko. Chukua huu.*
**huwa** usually; it is customary.
*Yusuf huwa amechelewa. Huwa wanagombana.*
**huyo** that; that one; that one we have been talking about; that one over there near you.
*Huyo alinisumbua sana.*
**huyu** this; this one.
*Huyu ni mvulana. Mpige huyu!*
**huzuni** (huzuni) being sad.
*Huzuni yake ilionekana kuwa kubwa.*
**huzunika** to be very sad.
*Niliposikia habari ile mbaya, nilihuzunika sana.*

# I

**i** it is; they are.
*Kalamu i karibu naye. Mimea i mirefu.*
**idara** (idara) a part of the government.
*Kaka yangu afanya kazi katika Idara ya Elimu.*
**idadi** (idadi) a number.
*Sikuweza kuhesabu vitu hivyo; vilikuwa bila idadi.*
**iga** to imitate or mimic—that is, to do something in the same way that someone else does that thing.
*Kasuku anaweza kuiga sauti ya binadamu.*
**igiza** to act out something, as in a play.
*Watoto walisoma mazungumzo vitabuni, kisha wakaigiza mazungumzo hayo.*
**ijapokuwa** even if.
*Ijapokuwa atanisihi, sitamsaidia.*
**Ijumaa** (Ijumaa) Friday.
*Ijumaa hufuata Alhamisi. Kila Ijumaa Ali huenda msikitini.*
**ikiwa** if.
*Ikiwa una pesa, nipe kidogo. Ikiwa hutaki, usichukue.*
**ila** except.
*Kila mtoto alisimama ila Hamisi. Nipe vitabu vile ila hicho kikubwa.*
**ile** that one over there; those ones over there.
*Lete kalamu ile. Angalia milima ile.*
**ili** so that.
*Nilimpa pesa ili aninunulie gazeti.*
**imani** (imani) faith; believing something.
*Nina imani na Mungu.*
**imara** (imara) strength; being strong.
*Alijenga ukuta mbaya usiokuwa imara.*
**imba** to sing.
*Maria aliimba wimbo mtamu.*
**imbia** to sing to someone or for someone.
*Watatuimbia nyimbo mbili.*
**inama** to bow; to bend down.
*Mti huu umeinama kwa sababu ya uzito wa matunda yake.*
**inamia** to bow to someone.
*Tulimwinamia Rais.*
**inamisha** to make something bend down.
*Uzito wa matunda uliinamisha mti.*
**ingawa** although.
*Ingawa kitabu kilikuwa ghali, nilikinunua. Anaweza kusoma ingawa ana umri wa miaka minne tu.*
**-ingi** many; a lot of something.
*Mwalimu husema maneno*

*mengi. Kuna watu wengi mjini Nairobi. Alikula uji mwingi. Tajiri huyo ana pesa nyingi.*

**ingia** to go in. *Watoto waliingia ndani ya nyumba.*

**ingilia** to go into something in a special way. *Watoto wasiingilie mambo ya watu wazima.*

**-ingine** another; other. *Niletee viatu vingine. Watu wengine wamefika. Alinipa papai hili na papai moja jingine.*

**ingiza** to make something or someone go in. *Aliingiza vitabu sandukuni.*

**injini** (injini) an engine. *Injini ya motokaa imeharibika.*

**inua** to lift up; to raise up. *Labda mtu mwenye nguvu ataweza kuinua jiwe hili.*

**inzi** (mainzi) a fly. *Mainzi huleta uchafu; wafukuze!*

**isha** to end; to finish. *Chakula kimekwisha; tumekula chote. Soda haijaisha.*

**ishara** (ishara) a sign which tells you that something is wrong or that something is going to happen. *Je, uliona ishara hiyo ya taa nyekundu?*

**ishi** to live; to stay. *Huyu mzee sana; ameishi miaka mingi.*

**ishirini** twenty. *Chukua shilingi hizi ishirini. Nataka viazi ishirini.*

**ita** to call. *Kwa nini uliniita?*

**itika** to answer when called. *Nilipomwita aliitika mara moja.*

**itwa** to be called. *Ameitwa na mwalimu. Yohana, unaitwa.*

**iva** to get ripe. *Matunda yote yameiva.*

# j

**ja** to come. *Anakuja sasa. Kwa nini haji?*

**jaa** to be full. *Chombo hiki kimejaa maziwa. Maziwa yamejaa chomboni.*

**jahazi** (majahazi) a kind of ship. *Tulipokwenda Mombasa tuliona majahazi mengi.*

**jali** to behave the right way towards something important or someone important. *Mwivi hakujali sheria, akafungwa jela.*

**jamaa** (jamaa) a number of people together; a family. *Hawa wote ni wa jamaa moja.*

**jamani** what someone calls the people he is speaking to when he wants to make them be like his family. *Jamani, nawaambieni tutajenga nchi yetu.*

**jambo** (mambo) a matter; something which happens to someone or which bothers someone. *Mambo hayo yalinisumbua sana.*

**jamhuri** (jamhuri) a republic—that is, a country in which the leader is chosen by the people. *Twapenda jamhuri yetu ya Kenya.*

**jamii** (jamii) a group of people or things. *Walifika wote jamii.*

**jana** (jana) yesterday. *Jana na juzi si kama ya leo. Maskauti walifanya kazi nyingi jana.*

**jani** (majani) a leaf. *Mti huu una majani mengi, madogo.*

**-janja** clever in a bad way.

*Kwa kawaida mwivi ni mtu mjanja. Siwapendi watoto hao wajanja.*

**Januari** (Januari) January.
*Mwezi wa Januari hufuata mwezi wa Desemba.*

**jaribio** (majaribio) trial; a kind of test.
*Majaribio hayo yalitusumbua sana.*

**jaribu** to try.
*Alijaribu kufungua mlango.*

**jasho** (jasho) sweat—that is, water which comes from all over your body when you are hot.
*Mfanyi kazi huyo anatoa jasho nyingi.*

**jaza** to make something be full.
*Nitajaza bilauri hii maji.*

**je** a word that someone says when he is about to ask a question.
*Je, bwana, unajua kusoma?*

**jela** (jela) jail; a kind of prison.
*Mwivi amefungwa jela.*

**jeneza** (jeneza) a kind of bed for carrying someone who has died to the place where his body will be put.
*Walichukua maiti kaburini kwa jeneza kubwa.*

**jenga** to build.
*Mkulima alijenga ukuta huu.*

**jengo** (majengo) a building.
*Nairobi kuna majengo mengi sana.*

**jeshi** (majeshi) an army.
*Majeshi ya Kenya hutulinda sisi.*

**jibu** to answer.
*Ukiniuliza nitajibu.*

**jibu** (majibu) an answer.
*Swali lako halina jibu.*

**jicho** (macho) an eye.
*Kila mtu huwa na macho mawili.*

**jificha** to hide yourself.
*Wanyama walijificha vichakani.*

**jifunza** to learn.
*Huyu anajifunza lugha ya Kiswahili.*

**jiko** (meko au majiko) a kitchen; a stove.
*Mpishi hufanya kazi jikoni.*

**jina** (majina) a name.
*Jina lake ni Hamisi.*

**jini** (jini au majini) a genie or fairy.
*Jini alinitisha sana. Kuna tofauti baina ya jini na shetani.*

**jino** (meno) a tooth.
*Jino langu ni baya; linaniuma.*

**jinsi** (jinsi) how something is done; the way something is done.
*Hivyo ndivyo jinsi alivyokuwa akishona.*

**jiografia** (jiografia) geography—that is, the study of the world and all its different countries and mountains and rivers and seas.
*Kitabu hiki cha jiografia kina ramani nyingi.*

**jioni** (jioni) evening or in the evening.
*Tulifika huku jana jioni.*

**jipu** (majipu) a boil—that is, a small, hard, swelled-up place on someone's body that hurts very much.
*Mgonjwa alisumbuliwa sana na majipu.*

**jirani** (jirani au majirani) a neighbour—that is, someone who lives near someone else.
*Huyu ni jirani yangu; nyumba yake iko karibu na nyumba yangu.*

**jitahidi** to try hard.
*Nilipojaribu mara ya kwanza nilishindwa lakini nikajitahidi nikafaulu.*

**jitenga** to move yourself or keep yourself away from everyone else.
*Hapo kale makabila ya Kenya*

*yalizoea kujitenga.*

**jitengenezea** to repair something for yourself or by yourself.
*Motokaa yake iliharibika, akajitengenezea mwenyewe.*

**jitoa** to put yourself forward so that you are ready to do some work.
*Tujitoe kwa nguvu kujenga nchi yetu ya Kenya.*

**jitu** (majitu) a giant.
*Yeye ni mkubwa kama jitu!*

**jivunia** to boast about something.
*Yeye hujivunia [illegible]li yake na mimi sipendi majivuno yake.*

**jiwe** (mawe) a stone.
*Watoto wakorofi walimtupia mbwa mawe.*

**jogoo** (majogoo) a cock.
*Nasikia jogoo akiwika.*

**jongoo** (majongoo) a millipede—that is, a creature like an insect which has very many legs; it does not bite.
*Siwezi kuhesabu miguu ya jongoo.*

**joto** being very hot.
*Kwenye jua kuna joto jingi sana.*

**jua** to know.
*Je, unajua jina lake? Anajua kucheza mpira.*

**jua** (majua) the sun; a sun.
*Jua ni kali leo. Kwa hakika nyota ni majua yaliyoko mbali sana na dunia hii yetu.*

**jukwaa** (majukwaa) a raised platform.
*Waziri alisimama kwenye jukwaa, akatoa hotuba yake.*

**Julai** (Julai) July.
*Mwezi wa Julai hufuata mwezi wa Juni.*

**julisha** to make someone know something.
*Nilimjulisha huyo jina langu.*

**juma** (majuma) a week.
*Mwaka huwa na majuma hamsini na mawili.*

**Jumamosi** (Jumamosi) Saturday.
*Yohana hapendi kufanya kazi Jumamosi.*

**Jumanne** (Jumanne) Tuesday.
*Mamangu huenda sokoni kila Jumanne.*

**Jumapili** (Jumapili) Sunday.
*Kila Jumapili Paulo huenda kanisani.*

**Jumatano** (Jumatano) Wednesday.
*Jumatano hufuata Jumanne.*

**Jumatatu** (Jumatatu) Monday.
*Kwa kawaida Jumatatu ni siku ya kazi.*

**jumba** (majumba) a large house or building.
*Tajiri huyo amenunua jumba kubwa.*

**jumbe** (majumbe) a headman or a chief.
*Huyu ndiye jumbe wetu.*

**Juni** (Juni) June.
*Mwezi wa Juni hufuata mwezi wa Mei.*

**juta** to be sorry about something.
*Nilimsumbua mamangu bure na sasa ninajuta.*

**juu** (juu) up; above; the top.
*Ndege alipumzika juu ya mti.*
*Tiara ilipaa juu kwa juu.*

**juzi** (majuzi) the day before yesterday.
*Sikumwona jana; nilimwona juzi tu.*

# k

**kaa** to stay.
*Nimekaa mjini Nairobi tangu mwaka wa 1966.*

**kaa** (kaa) a crab—that is, a little creature which lives on the beach or in the sea.
*Nilipotembea ufukoni kwa pwani niliona kaa wengi sana.*

**kabati** (kabati au makabati) a cupboard.
*Makabati haya ni makubwa sana.*

**kabila** (makabila) a tribe.
*Huku Kenya kuna makabila mengi. Huyu ni rafiki yangu, kabila lake Pokot.*

**kabisa** quite; altogether.
*Nimechoka kabisa.*

**kabla** before.
*Nadhani ataondoka kabla sijafika.*

**kaburi** (makaburi) a grave—that is, the place where the dead body of someone is put.
*Maiti ilipelekwa kaburini.*

**kadhalika** and so on; in the same way.
*Hesabu moja, mbili, tatu, na kadhalika. Mtoto huyu mrefu na huyo kadhalika.*

**kadha wa kadha** a few; some.
*Nilikwenda Kapenguria, nikaona watu kadha wa kadha si wengi.*

**kadiri** (kadiri) how much or how many of something.
*Niliona kadiri ya watu thelathini hivi. Kadiri gani?*

**kagua** to examine; to look at carefully.
*P.C. alikagua Gadi ya Heshima.*

**kahawa** (kahawa) coffee.
*Alikunywa kahawa vikombe viwili.*

**kaka** (kaka) brother.
*Huyu ni kaka yangu.*

**kaki** (kaki) khaki; a kind of cloth.
*Kaputula hizi ni za kaki.*

kaa

**kalamu** (kalamu) a pen or pencil.
*Andika kwa kalamu hii.*

**kale** a long time ago.
*Watu wa kale walitumia vifaa vya mawe.*

**kalenda** (kalenda) a calendar—that is, something like a book which is hung on the wall and which shows all the days and months in a year.
*Nimenunua kalenda mpya kwa sababu leo ni siku ya mwisho ya mwaka.*

**-kali** sharp; fierce; bitter; being someone who gets angry easily; not gentle at all.
*Hiki ni kisu kikali. Daktari alinipa dawa kali. Jua ni kali leo. Maneno yake yalikuwa makali. Huyo ni mtu mkali sana.*

**kama** to squeeze; especially to squeeze milk from a cow.
*Alikama ng'ombe zake, akapata maziwa lita thelathini.*

**kama** like; if.
*Naona hiki ni kama hicho. Kama unataka, tutakwenda pamoja.*

**kamata** to catch hold of; to grasp.
*Askari polisi alimkamata mwivi.*

**kamba** (kamba) a rope.
*Kamba hii ni ndefu sana.*

**kambi** (kambi au makambi) a camp.
*Tulipiga kambi yetu kando ya mto.*

**kamili** whole.
*Niambie habari kamili. Sitaki mguu wa kiti; nataka kiti kamili.*

**kamilisha** to finish; to put in all the parts that are not there.
*Kamilisha zoezi hili.*

**kamua** to squeeze; especially to squeeze milk from a cow.
*Yeye hukamua ng'ombe zake mara mbili kila siku.*
*Alikamua nguo zake.*

**kamwe** not at all; not once.
*Sijamwona kamwe.*

**kando** (kando) the edge or side, especially of a river or sea.
*Kando ya mto kulikuwa na hema tatu.*

**kanga** (kanga) a piece of cloth that women wear as a kind of dress.
*Dada yangu alinunua kanga mpya.*

**kaniki** (kaniki) a dark blue cloth.
*Kaniki hii imepasuka.*

**kanisa** (makanisa) a church.
*Jumapili watu wengi huenda kanisani.*

**kanyaga** to step on something; to stamp on something with your feet.
*Kanyaga mdudu huyo!*

**kanzu** (kanzu) a kind of long dress with long sleeves worn by men.
*Yusuf amevaa kanzu nzuri.*

**kapu** (makapu) a large basket.
*Je, una nini katika kapu lako?*

**kaputula** (kaputula) shorts.
*Wavulana wa skuli hii huvaa kaputula nyekundu.*

**karamu** (karamu) a party or feast—that is, when lots of people meet together to dance and sing and eat.
*Kesho kutakuwa na karamu kubwa ya kupendeza.*

**karani** (makarani) a clerk.
*Karani huyu amekataa kunisaidia.*

**karanga** (karanga) a ground nut—that is, a kind of seed which grows under the ground and which is good to eat.
*Watoto hupenda kula karanga kama hizi.*

**karatasi** (karatasi) paper.
*Alifanya tiara kwa kutumia karatasi na vijiti na gundi.*

**karibia** to come near to something or someone.
*Nilipomkaribia mbwa alianza kubweka.*

**karibisha** to make someone move close to something; to invite someone to move closer to something.
*Tulimkaribisha aingie ndani ya nyumba yetu.*

**karibu** near; close.
*Simama hapa karibu na mimi.*

**karibu** almost.
*Alikuwa karibu kufa. Aliwapiga karibu awaue.*

**karibu** come in!
*Alisema, 'Hodi?' Nikasema, 'Karibu.'*

**kasa** less; take away.
*Alifika saa mbili kasa robo.*

**kasirika** to be angry.
*Mwalimu amekasirika kwa sababu watoto hawafanyi kazi kwa bidii.*

**kasirisha** to make someone angry.
*Mtoto huyo alimkasirisha mwalimu.*

**kaskazini** north; toward your left if you are facing where the sun rises.
*Nchi ya Ethiopia iko upande wa kaskazini wa nchi ya Kenya.*

**kasoro** less; take away.
*Kengele ililia saa saba kasoro dakika kumi.*

**kasuku** (kasuku) a parrot.
*Kasuku huyu anaweza kuiga sauti ya binadamu.*

kasuku

**kata** to cut.
*Ni nani aliyekata kamba hii?*

**kataa** to refuse; to say no.
*Nilimwamuru aende lakini akakataa.*

**katakata** to cut something into little pieces.
*Mama alikatakata nyama.*
**katani** (katani) sisal.
*Kamba hii ni ya katani.*
**kataza** to forbid—that is, to tell someone that he should not do something.
*Nilimkataza asiende.*
**kati** the middle; between or among.
*Aliketi kati ya rafiki zake.*
**katika** in.
*Weka kitabu katika kabati.*
**katikati** the middle; between or among.
*Swala alisimama katikati ya miti ile.*
**kauka** to get dry.
*Nilianika nguo juani, zikakauka.*
**kausha** to make something get dry.
*Jua limekausha nguo zote.*
**-kavu** dry.
*Shati langu ni kavu sasa. Hapa ni pakavu sana. Vitambaa vile ni vikavu.*
**kawa** (kawa au makawa) a dish cover—that is, a thing that is put over the top of a dish.
*Uliweka wapi kawa ya chombo hiki?*
**kawaida** (kawaida) custom—that is, a general rule to do something a certain way because it has been done that way for a long time.
*Kwa kawaida wanawake hupika chakula.*
**kawia** to take a long time; to be late.
*Nendeni sasa; msikawie hata kidogo!*
**kazi** (kazi) work.
*Yeye amefanya kazi nyingi.*
**keki** (keki) a cake.
*Mama alitengeneza keki, watoto wakazila zote.*
**kelele** (kelele au makelele) noisy sounds.
*Watoto wale wanafanya makelele mengi.*
**kenge** (kenge) a kind of very big lizard.
*Naogopa kenge kama yule.*
**kengele** (kengele) a bell.
*Kengele ya skuli ilipolia, tuliingia ndani ya darasa.*
**kesho** (kesho) tomorrow.
*Tutakwenda mjini kesho.*
*Yusuf alifika siku hiyo na Abudu kesho yake.*
**kesho kutwa** the day after tomorrow.
*Tutakwenda kesho na kurudi kesho kutwa.*
**keti** to sit.
*Ameketi kitini.*
**ki** it is.
*Kitabu ki karibu nawe.*
**kiasi** how much or how many of something; a little bit of something.
*Alinipa kiasi cha chakula chake.*
**kiatu** (viatu) a shoe.
*Amevaa viatu vyake vipya.*
**kiazi** (viazi) a sweet potato.
*Mamangu amepika viazi hivi viwili.*
**kibanda** (vibanda) a little house or a little hut.
*Tuliona kibanda kidogo kando ya mto.*
**kiberiti** (viberiti) a matchbox—that is, a box full of little sticks called matches which make fire when they are rubbed against something.
*Nilinunua viberiti vitatu dukani.*
**kibuyu** (vibuyu) a gourd.
*Kibuyu hiki kina maji ndani yake.*
**kichaka** (vichaka) a group of small trees and bushes.
*Vifaru hukaa vichakani.*
**kichwa** (vichwa) a head.
*Kichwa chake ni kikubwa sana.*
**kidevu** (videvu) chin.

*Yeye ana kidevu kikubwa.*

**kidogo** a little
*Nipe sukari kidogo. Sukuma kidogo.*

**kidokezi** (vidokezi) secret words or a secret sign to tell someone something.
*Nilisikia kidokezi chake.*

**kidole** (vidole) a finger.
*Mkono wangu una vidole vitano.*

**kidonda** (vidonda) a little sore—that is, a little place on your body that hurts.
*Kidonda hiki kinanisumbua sana.*

**kienyeji** local; not strange or foreign; the way something has been done in a country for a long time.
*Ugali ni chakula cha kienyeji.*

**kifaa** (vifaa) a useful thing; a tool.
*Vitu hivi vilikuwa vifaa vya watu wa zamani.*

**kifagio** (vifagio) a broom or brush.
*Mwalimu anataka kifagio kile.*

**kifaranga** (vifaranga) a chick; a baby bird.
*Nilimwona mama kuku pamoja na vifaranga wake wanane.*

**kifaru** (vifaru) a rhino—that is, a big animal with two horns on its nose.
*Niliwaona vifaru wawili karibu na Tsavo.*

**kifaru**

**kifo** (vifo) death—that is, when someone dies.
*Nilisikia habari ya kifo chake.*

**kifua** (vifua) someone's chest.
*Kifua chake kilionekana kwa sababu shati lake lilikuwa limepasuka vibaya.*

**kifudifudi** the way someone is lying down when his face is toward the ground.
*Nilimwona amelala kifudifudi.*

**kifungo** (vifungo) a button.
*Shati lake lina vifungo vinne.*

**kifungu** (vifungu) a little pile of something; parentheses—that is, marks like these: ( ).
*Alinipa kifungu cha vitabu.*
*Neno hili ni katika vifungu: (neno).*

**kifuniko** (vifuniko) a lid or top.
*Chupa hii ina kifuniko kidogo.*

**kifurushi** (vifurushi) a kind of little bag or bundle, such as a piece of paper folded to make a little bag or bundle.
*Nilinunua bahasha, kifurushi kimoja.*

**kijana** (vijana) a young boy or girl.
*Vijana wa siku hizi hawana adabu kama wale wa zamani.*

**kijani** green.
*Napenda rangi ya kijani kibichi kuliko rangi nyekundu.*

**kijiko** (vijiko) a spoon.
*Kijiko changu ni kichafu.*

**kijiji** (vijiji) a little village.
*Nakaa katika kijiji kidogo.*

**kijiti** (vijiti) a stick.
*Kijiti hiki ni kifupi.*

**kikapu** (vikapu) a basket.
*Nilimpelekea mamangu kikapu chake.*

**kike** like a girl or woman.
*Hawa ni watoto wa kike.*

**kiko** (viko) a pipe.
*Kuna tumbako katika kiko chake.*

**kikombe** (vikombe) a cup.
*Kikombe changu kimevunjika.*

**kikosi** (vikosi) a group of soldiers.
*Kule kuna kikosi cha askari.*

**kikundi** (vikundi) a group of

people or animals.
*Kikundi cha watu kinatukaribia*
**kila** every.
*Kila mtu awe huru. Huyo anataka kununua kila kitu. Kila niendako nakukuta wewe.*
**kilabu** (vilabu) a club—that is, a place where people go to dance and drink beer.
*Usiingie katika kilàbu hicho!*
**kile** that one over there.
*Lete kitabu kile.*
**kilele** (vilele) the peak of a mountain.
*Batian na Nelion na Lenana ni vilele vya mlima wa Kenya.*
**kilemba** (vilemba) a turban.
*Hajui kupiga kilemba vizuri.*
**kilo** (kilo) a kilogram—that is, a measure of weight; about two pounds.
*Nitanunua unga kilo mbili.*
**kima** (kima) a kind of monkey.
*Naona kima watatu mtini.*
**kimbia** to run; to run away.
*Watoto wote walikimbia.*
*Usikimbie; tembea polepole.*
**kimbilia** to run toward something or someone.
*Watoto walimkimbilia baba yao.*
**kimbiza** to make someone run away.
*Mtoto aliwakimbiza kuku kwa kuwatupia mawe.*
**kimetameta** (vimetameta) a sparkle or shining.
*Napenda kimetameta cha nyota.*
**kimetameta** (vimetameta) a firefly—that is, a little insect that gives off light.
*Vimetameta ni wadudu wadogo ambao humetameta usiku.*
**kimya** in a silent way.
*Watoto walinyamaza kimya.*
**kina** people of a certain sort; a kind of people.
*Kina wavulana waje hapa.*
**kinu** (vinu) a mortar—that is, a piece of wood whose top is like the inside of a bowl; it is used for pounding grain in.
*Kinu hiki ni kikubwa.*
**kinyonga** (vinyonga) a chameleon.
*Anna alimwona kinyonga mmoja barabarani.*
**kinyozi** (vinyozi) a barber—that is, someone who cuts other people's hair.
*Kinyozi huyo alikata nywele zangu kwa kutumia mkasi na wembe.*
**kinyume** opposite.
*Joto ni kinyume cha baridi.*
**kinywa** (vinywa) mouth.
*Kinywa chake kimejaa chakula.*
**kiongozi** (viongozi) a leader.
*Kiongozi alituongoza nasi tulimfuata.*
**kioo** (vioo) a piece of glass or a mirror.
*Kioo hiki ni kikubwa.*
**kipande** (vipande) a small piece of something.
*Nipe kipande cha nyama yako.*
**kipepeo** (vipepeo) a butterfly.
*Vipepeo wengi wanaruka hewani.*

**kipepeo**

**kipindi** (vipindi) a period of time—that is, some minutes or hours; part of a football game.
*Timu yetu ilipata mabao mawili katika kipindi cha pili.*
**kipofu** (vipofu) someone blind—that is, someone who cannot see.

*Yeye ni kipofu; hawezi kuona.*

**kiri** to admit or confess—that is, to say that you have done something wrong.
*Aliposhtakiwa alikiri makosa hayo.*

**kiroboto** (viroboto) a flea—that is, a little insect which bites animals and people and which can jump high.
*Niliumwa na viroboto wengi.*

**kisa** (visa) a story.
*Aliwasimulia watoto visa vya kupendeza.*

**kisanduku** (visanduku) a little box.
*Kisanduku hiki ni kidogo sana.*

**kisasi** (visasi) revenge—that is, doing something bad to someone because he has done something bad to you.
*Vitendo vya kisasi si vizuri.*
*Nilipasua shati lake na sasa ana kisasi na mimi; anapasua shati langu.*

**kisha** afterwards.
*Nililala usingizi, kisha nikaamka.*

**kisima** (visima) a water-hole; a place to get water.
*Alikwenda kisimani, akateka maji.*

**kisiwa** (visiwa) an island.
*Tulisafiri kwa mashua tukafika kwenye kisiwa kikubwa.*

**kisu** (visu) a knife.
*Nataka kisu cha kukatia nyama.*

**kitabu** (vitabu) a book.
*Napenda kusoma vitabu kama hivi.*

**kitako** on your bottom.
*Afadhali ukae kitako sasa.*

**kitambaa** (vitambaa) a small cloth or handkerchief.
*Kitambaa changu kimepasuka.*

**kitambo kidogo** in a little while.
*Mwalimu asema kwamba atarudi kitambo kidogo.*

**kitana** (vitana) a comb.
*Amina amepoteza kitana chake cheusi.*

**kitanda** (vitanda) a bed.
*Amelala kitandani kwa sababu ni mgonjwa.*

**kitanzi** (vitanzi) a loop—that is, a circle of thread or rope.
*Alifanya kitanzi kikubwa katika kamba.*

**kitendo** (vitendo) an action—that is, something someone does, such as to move, to dance, to throw.
*Kitendo chake kilimkasirisha mwalimu.*

**kiti** (viti) a chair.
*Niliona kiti kizuri, nikaketi chini.*

**kitu** (vitu) a thing.
*Kitu gani hiki?*

**kitumbua** (vitumbua) a fritter—that is, a kind of food usually cooked in a frying pan; it is good to eat.
*Babangu alininunulia vitumbua viwili.*

**kitunguu** (vitunguu) an onion.
*Mama alinunua vitunguu kumi na vitatu.*

**kituo** (vituo) a place to stop or rest; a special place.
*Nilinunua miti hii michanga kwenye kituo cha miti.*

**kiu** (kiu) being without water; what someone feels when he is thirsty.
*Nasikia kiu; nipe maji.*

**kiumbe** (viumbe) a creature.
*Mungu aliumba viumbe vyote.*

**kiume** like a boy or man.
*Mwanamke alizaa mtoto wa kiume. Wavulana walishindana kiume.*

**kiuno** (viuno) waist.
*Amevaa mshipi kiunoni.*

**kivuli** (vivuli) a shadow or a place in the shade.
*Napenda kulala kwenye kivuli cha mti.*

**kiwanda** (viwanda) a factory.
*Kaka yangu hufanya kazi katika kiwanda kile kikubwa.*

**kiwanja** (viwanja) a flat place, a piece of ground.
*Watoto walikutana kwenye baada ya mwezi mmoja.*

**kiwavi** (viwavi) a caterpillar.
*Kiwavi huyu atageuka kipepeo baada ya mwezi mmoja.*

**kizazi** (vizazi) birth—that is, when someone begins to live.
*Aliniambia habari za kizazi cha mwanawe.*

**-ko** is there; are there.
*Baba yuko nyumbani. Vitabu viko kabatini. Chungwa liko pale. Mkeka uko sakafuni.*

**koa** (koa au makoa) a snail.
*Koa huyu mkubwa sana.*

**kobe** (makobe) a tortoise.
*Kobe kama huyu hutembea polepole.*

**kofi** (makofi) the flat part of a hand.
*Aliposhinda, tulipiga makofi kwa furaha.*

**kofia** (kofia) a hat.
*Mwalimu amevaa kofia yake.*

**kohoa** to cough.
*Tulikohoa sana kwa sababu ya vumbi.*

**kojoa** to urinate—that is, to pass water out of your body.
*Watoto wachanga hukojoa po pote.*

**koma** to stop.
*Mpira ulibingirika kidogo, ukakoma.*

**kombe** (kombe au makombe) a large cup or curved dish; a sea-shell.
*Nilipotembelea pwani niliona kombe nyingi. Mkimbiaji alipokea kombe la ushindi.*

**konda** to get thin.
*Hakula chakula kwa siku sita, akaanza kukonda.*

**kondoo** (kondoo) a sheep.
*Kondoo huyu ni wangu.*

**konyeza** to wink; to make a secret sign to someone.
*Maria alinikonyeza kwa macho.*

**koo** (koo) throat—that is, the front of someone's neck.
*Vumbi limeniingia kooni.*

**kopo** (makopo) a loan—that is, money or something else which someone gives you for a while but which you are supposed to give back later.
*Nimepata kopo kubwa lakini nitamlipia shilingi hamsini kila mwezi.*

**koroboi** (koroboi) a little lamp.
*Kwa nini hujawasha koroboi?*

**koroboi** (koroboi) a bad name for someone who has changed his African ways to non-African ways.
*Usiniite koroboi; mimi hufuata desturi ya kiafrika.*

**-korofi** very very bad.
*Askari wamemfunga mtu huyo mkorofi. Mimi huogopa watu wakorofi.*

**kosa** to do something wrong; to be without something.
*Alikosa; halafu akakiri kufanya makosa. Kalamu hii inakosa wino.*

**koti** (makoti) a coat.
*Koti langu ni jekundu.*

**kua** to grow or to grow up.
*Kondoo hawa wanakua vizuri.*

**kubali** to agree; to say yes.
*Nataka twende leo nawe umekubali.*

**-kubwa** big or large.
*Mwanamume huyu ni mkubwa. Nitanunua meza kubwa. Alinionyesha viazi vikubwa sana.*

**kucha** (tazama *cha*)

**kuchakulo** (kuchakulo) a squirrel—that is, a kind of small animal with a bushy tail. (See the picture on page 36.)
*Kuchakulo wale wawili walikula njugu karanga zangu.*

kuchakulo

**kufa** (tazama *fa*)

**kufuli** (kufuli) a padlock—that is, a metal thing which is used to keep a door or box shut; it is opened with a key.
*Mlango umefungwa kwa kufuli hii.*

kufuli



**kuja** (tazama *ja*)

**kuku** (kuku) a chicken; a hen.
*Kuku wangu ametaga mayai manne.*

**kula** (tazama *la*)

**kule** over there.
*Hamisi yuko kule.*

**kulia** right.
*Huu ni mkono wangu wa kulia. Fuata njia iendayo upande wa kulia.*

**kuliko** than.
*Mtoto huyu ni mkubwa kuliko yule.*

**kumbe** a word which someone says when he is surprised.
*Kumbe ni wewe uliyeiba kitabu changu!*

**kumbikumbi** (kumbikumbi) a rain-ant—that is, a kind of small insect with wings which appears when the rains start.
*Watu wa huku hupenda kula kumbikumbi.*

**kumbikumbi**

**kumbuka** to remember.
*Sasa nimekumbuka jina lake nililosahau jana.*

**kumbusha** to make someone remember something; to remind.
*Nilimkumbusha ahadi yake.*

**kumi** ten.
*Nunua visu kumi. Nipatie matunda kumi na mawili. Somo la kumi ni somo gumu.*

**kuna** to scratch.
*Niliumwa na kiroboto, nikakuna mguu wangu.*

**kundi** (makundi) a group.
*Kule kuna kundi la watu.*

**kunguni** (kunguni) a bug; a kind of small insect.
*Kunguni huyu ni mdogo.*

**kunguru** (makunguru) a crow, especially a big black and white crow.
*Kunguru anaruka juu, hewani.*

**kunja** to fold.
*Kwa nini umekunja karatasi hizi?*

**kunywa** (tazama *nywa*)
**kupa** (tazama *pa*)
**kuputu** the sound that a horse's or buck's hoofs make when it runs.
*Farasi alikimbia kuputu kuputu kuputu.*
**kusanya** to gather together.
*Mwalimu amekusanya vitabu vyote.*
**kusanyika** to be gathered together.
*Watu wale wamekusanyika ili wasikilize hotuba ya Rais.*
**kushoto** left.
*Fuata barabara iendayo upande wa kushoto.*
**kusini** south; toward your right if you are facing where the sun rises.
*Nchi ya Tanzania iko upande wa kusini wa nchi ya Kenya.*
**kusudi** (makusudi)-aim.
*Hilo ndilo kusudi lake.*
**kusudi** so that.
*Amekuja kusudi atusaidie. Nimefanya kazi kusudi nipate mshahara. Anahudhuria skuli kusudi aweze kusoma na kuandika.*
**kuta** to meet.
*Nilimkuta rafiki yangu sokoni.*


kunguni

**kutana** to meet together.
*Sisi sote tutakutana uwanjani kesho. Nafikiri nitakutana nanyi kesho kutwa.*
**kutoka** (tazama toka).
**kutoka** from.
*Tutasafiri kutoka Kisii mpaka Ki'ale. Alifanya kazi kutoka saa moja mpaka saa kumi.*
**-kuu** great.
*Nairobi ni mji mkuu wa Kenya. Ramadhani ni mkaguzi mkuu kiwandani. Angalia kiazi hiki kikuu.*
**-kuukuu** old and no good any more.
*Motokaa yake ni kuukuu; haiwezi kwenda. Sitaki kitu hicho kikuukuu.*
**kuwa** to be.
*Alikuwa mtoto tu. Nitakuwa mwalimu wenu.*
**kuwa** that.
*Nilimwambia kuwa nitamsaidia.*
**kuza** to make something grow bigger.
*Dawa hii itakuza ng'ombe zako.*
**kwa** by; for; with; through.
*Tutakwenda kwa miguu. Umekuja kwa nini? Alinikata kwa kisu. Tuliangalia kwa dirisha.*
**kwaa** to knock your foot against something.
*Nilijikwaa mguu, nikaanguka chini.*
**kwa heri** goodbye.
*Alipoondoka alisema, 'Kwa heri'.*
**kwamba** that.
*Alisema kwamba atafika kesho.*
**kwanza** first.
*Mtoto huyu alikuwa wa kwanza katika mashindano. Tusome kitabu hiki kwanza na hicho baadaye.*
**kweli** truth.
*Yeye husema kweli. Nafikiri maneno haya ni ya kweli.*
**kwisha** (tazama *isha*)

# l

**la** to eat.
*Amekula matunda yote. Sijala chakula cho chote.*
**la** no.
*Nilimwuliza kama atakwenda kesho, akasema, 'La, sitakwenda'.*
**labda** perhaps.
*Labda wageni watafika kesho.*
**laini** soft or thin and fine.
*Nitanunua nguo laini kama hii. Kitambaa hiki ni laini.*
**laki** to go to meet someone.
*Wananchi wengi walikwenda kumlaki balozi.*
**lakini** but.
*Nataka kwenda sinema lakini sina pesa.*
**lala** to lie down; to go to sleep.
*Hamisi amelala usingizi.*
**lamba** to lick.
*Mbwa alilamba mkono wangu.*
**laza** to make someone lie down.
*Daktari alimlaza mgonjwa kitandani.*
**lazima** necessary; must be done.
*Ni lazima turudi sasa.*
**lazimu** to be made to do something.
*Yanilazimu kufanya kazi hii.*
**lea** to raise a child; to help a child grow up.
*Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.*
**legea** to be loosened.
*Kamba ililegea, mfungwa akatoroka.*
**legeza** to loosen.
*Skauti alilegeza kamba kidogo.*
**lengo** (malengo) a target—that is, something which is aimed at.
*Lengo letu ni kuchanga shilingi elfu mbili.*
**leo** (leo) today.
*Sikuenda jana lakini naenda leo.*
**leta** to bring.
*Umeleta pesa? Lete maziwa!*
**letea** to bring to someone.
*Utaniletea kitabu changu? Tuletee chai!*
**li** it is.
*Chungwa li karibu naye.*
**-li-** is; are; am.
*Huyu ni mtu aliye na njaa. Nataka kitabu kilicho na picha nzuri. Mimi, niliye rafiki yako, nitakusaidia. Hizi ni meza zilizo na miguu mitatu.*
**lia** to cry.
*Mtoto alianguka, akalia.*
**likizo** (likizo au malikizo) a holiday.
*Wanafunzi hupenda siku za likizo.*
**lile** that one over there.
*Nataka tunda lile.*
**lima** to dig land before you plant it; to dig.
*Ni nani watakaolima shamba?*
**limau** (malimau) a lemon—that is, a kind of fruit like a yellow orange which tastes sour.
*Nenda sokoni ukaninunulie malimau manne.*
**linda** to protect; to do the work of a guard.
*Kazi ya mlinzi ni kulinda wevi wasiibe cho chote.*
**linganisha** to compare.
*Mwalimu alilinganisha miwani yangu na miwani yake.*
**lini** when?
*Ulifika lini? Wataondoka lini?*
**lipa** to pay.
*Ni vizuri kulipa deni lako. Umelipa ada za skuli?*
**lisha** to make someone eat something; to feed.
*Yohana huwalisha ng'ombe zake nyasi.*
**lita** (lita) a litre—that is, a

measure of how much, about a pint.
*Alinunua maziwa lita tatu.*

**livu** (livu) leave, a holiday.
*Mfanyi kazi alipata livu, akaenda pwani kwa mapumziko.*

**loo** a word that someone says when he is surprised or happy.
*Loo! Kuna dhahabu ndani ya sanduku!*

**lori** (malori) a lorry.
*Dereva huyu anajua kuendesha hata lori kubwa.*

**lowa** to get all wet.
*Alianguka mtoni, akalowa kabisa.*

**lugha** (lugha) a language—that is, a way of speaking which a child learns from his mother and father.
*Napenda kusema kwa lugha ya Kiswahili.*

# m

**m** you all are.
*Ninyi m tayari.*

**maana** (maana) a reason or cause—that is, why something was done or is done.
*Alifanya kazi kwa maana ya dada yake aliyekuwa hospitalini. Sikuweza kuendelea kwa maana nilikuwa na kiu. Unajua maana yake?*

**maandamano** a procession—that is, a group of people or animals or things moving along together in a line, one after another.
*Maandamano makubwa yalipitia Njia ya Harambee.*

**maarifa** (maarifa) knowledge or news.
*Alituambia maarifa hayo aliyoyapata mjini.*

**Machi** (Machi) March.
*Mwezi wa Machi hufuata mwezi wa Februari.*

**machozi** tears—that is, drops of water which come from someone's eyes when he is crying.
*Alipolia, machozi yalimtoka machoni.*

**madaraka** responsibility—that is, having power to do something and the duty to do it.
*Siku ya Madaraka ni tarehe gani? Sisi tuna madaraka ya kujitawala.*

**madhumuni** (madhumuni) aim.
*Uhuru wa biashara ni madhumuni yetu.*

**madini** (madini) metal.
*Dhahabu ni namna ya madini.*

**madoadoa** small dots of black or small dots of some other colour.
*Ngozi ya chui ina madoadoa.*

**maelezo** explanation—that is, words which tell what something means, or what it is like, or what it does, so that people can understand it.
*Mwalimu alinieleza jambo hilo, nikafahamu maelezo yake.*

**maendeleo** progress—that is, going on or going forward.
*Nchini Kenya kumekuwa na maendeleo mengi tangu 1963.*

**mafuta** cooking oil or paraffin.
*Niletee mafuta ya taa.*

**magharibi** west, toward where the sun sets.
*Nchi ya Uganda iko upande wa magharibi wa nchi ya Kenya.*

**mahali** (mahali) place.
*Hapa ndipo mahali pazuri.*

**mahali pa** instead of.
*Alinifukuza mahali pa kunisaidia. Tulipewa maji mahali pa chai.*

**mahindi** maize seeds.
*Mkulima aliuza mahindi, magunia hamsini.*

**maisha** life, the time when someone or some animal or some plant is alive.
*Katika maisha yake yote alikuwa mtu mwema.*

**maiti** (maiti) the body of someone who has died.
*Alikufa na maiti yake ikazikwa.*

**maji** water.
*Nipe maji; nina kiu sana.*
*Napenda kunywa maji ya machungwa.*

**majimaji** damp; a little bit wet.
*Bata hupenda kula chakula cha majimaji.*

**majira** (majira) a space of time; the time for something, a time of the year.
*Hakuna mtu awezaye kutawala majira ya mvua.*

**majivu** ashes—that is, the black or grey stuff that is left after something has burned.
*Tulichoma siafu kwa majivu ya moto.*

**majivuno** words which someone says when he is boasting.
*Simpendi Hassan kwa sababu ana majivuno mengi.*

**makaa** charcoal—that is, the sort of coal that is made by burning wood that is covered by soil.
*Makaa ni meusi.*

**makamasi** mucus—that is, the stuff like thick water that someone has in his nose if he has a cold.
*Mtoto alifuta makamasi.*

**makao** a place where people or animals stay.
*Mchwa hujenga makao ya udongo.*

**makasi** (makasi) scissors.
*Makasi haya ni yangu.*

**makini** in a way that is careful and not fast or excited.
*Alichungulia sarafu hiyo kwa makini.*

**makosa** errors; things which have been done wrong.
*Nisamehe baba; nimefanya makosa.*

**makuti** leaves from palm trees which are sometimes used to make the roof of a house.
*Mapaa ya nyumba zile ni ya makuti.*

**mali** (mali) anything which someone has, such as money, a house, clothes.
*Vitu hivi vyote ni mali ya tajiri yule.*

**malidadi** (malidadi) pretty marks on something, such as cloth; someone who is dressed very very well.
*Napenda nguo hii kwa sababu ya malidadi yake. Kweli, huyo ni malidadi.*

**maliza** to finish.
*Nimemaliza kazi yangu.*

**malkia** (malkia) a queen.
*Yule ni malkia wa nchi hiyo.*

**mama** (mama) a mother.
*Mama yangu anipenda sana.*

**manati** (manati) a catapult—that is, a little thing which is used to throw stones through the air.
*Umeona manati yangu?*

**manjano** (manjano) a kind of powder which is a yellow colour.
*Napenda rangi ya manjano kuliko rangi nyingine zote.*

**manyoya** wool or feathers or fur.
*Kondoo huwa na manyoya mengi.*

**maombi** prayers.
*Alitoa maombi yake msikitini.*

**maonyesho** a show.
*Tulipofika kwenye maonyesho ya ukulima, tuliona mambo mengi.*

**maovu** anything very bad or wicked.
*Nilimtenda mema, lakini akanitenda maovu.*

**mapema** early.

*Umefika mapema. Niliamka asubuhi na mapema.*

**mashindano** a competition or race.
*Ni nani aliyeshinda katika mashindano hayo?*

**mara** (mara) a time or times; immediately.
*Nilibisha mlango mara tatu.*
*Mara aliondoka.*

**marahaba** hello.
*'Shikamoo mzee'. 'Marahaba mtoto'.*

**marehemu** (marehemu) someone who has died.
*Tukumbuke marehemu Tom Mboya. Mtu aliyekufa huitwa marehemu.*

**marufuku** to be kept from doing something or from being somewhere.
*Mtu huyo mbaya alipigwa marufuku; hataweza kuingia katika Kenya tena.*

**mashariki** east, toward where the sun rises.
*Nilizaliwa katika Afrika ya Mashariki.*

**mashine** (mashine) a machine.
*Niliingia kiwandani, nikaona mashine nyingi.*

**mashirika** working together; a group of people working together.
*Watu wa mashirika hayo wamejisaidia sana.*

**mashua** (mashua) a kind of small boat.
*Tutasafiri kwa mashua hii yangu.*

mashua



**masika** (masika) the time of year when it rains a lot.
*Mvua ya masika imeanza sasa.*

**maskini** (maskini) someone who is very poor.
*Nitamsaidia huyu maskini.*

**matata** trouble.
*Sipendi matata kama haya!*

**mate** saliva—that is, the stuff like water which people have in their mouths.
*Yaya alifuta uso wa mtoto mchanga kwa sababu ulikuwa na mate.*

**matokeo** result—that is, something that happens because of something else.
*Matokeo ya safari yake yalikuwa ni mabaya sana.*

**matope** mud.
*Mvua ikinyesha, barabara hii itageuka matope tupu.*

**matumizi** things which are needed for someone to live, such as food and clothes.
*Maskini huyu hana matumizi.*

**maumivu** an ache or hurt; something which feels painful.
*Mgonjwa huyo ana maumivu kichwani.*

**mavi** dung—that is, the stuff which animals leave on the ground; it is sometimes used as fertilizer.
*Weka mavi ya ng'ombe shambani. Mbwa yule anaanza kunya mavi; mfukuze asichafue kiwanja chetu.*

**mavuno** a harvest—that is, what someone gets when he gathers together all that he has grown on his farm.
*Mwaka huu wakulima wamepata mavuno mengi.*

**mazao** something which is grown or got on a farm, such as maize or eggs or cows.
*Mkulima akitaka pesa, huuza mazao aliyoyapata shambani.*

**maziko** burial—that is, when a dead body of someone is put in a hole in the ground.
*Watu wengi walihudhuria maziko ya marehemu.*

**mazishi** all the things that are done before and after someone's body is put into the ground.
*Sijaona mazishi kama hayo uliyoyaona.*

**maziwa** milk.
*Watoto hupenda kunywa maziwa.*

**mazoea** a habit—that is, something which someone does so often that he does not even think about it any more.
*Alikuwa na mazoea ya kulala mapema na kuamka mapema.*

**mazungumzo** talk.
*Walizungumza, nami nilisikia mazungumzo yao.*

**mbaazi** (mbaazi) a kind of pea.
*Sipendi kula mbaazi.*

**mbalamwezi** the light of the moon which helps people to see at night.
*Kulikuwa na mbalamwezi usiku huo; kwa hivyo niliweza kuona vizuri.*

**mbali** far.
*Swala amekimbia mbali sana.*
*Mti ule uko mbali na hapa.*

**mbalimbali** various; different.
*Ana vitu mbalimbali.*

**mbega** (mbega) a kind of monkey.
*Mbega wengi hukaa kwenye mlima wa Elgon.*

**mbegu** (mbegu) a seed.
*Mkulima alipanda mbegu nyingi.*

**mbele** (mbele) something before; in front; forwards; some time ago.
*Mbele ya mti kulikuwa na nyasi tupu. Tuliendelea mbele. Mzee huyu anakumbuka siku za mbele.*

**mbili** two.
*Nataka karatasi mbili. Alihesabu, 'Moja, mbili, tatu, nne, tano.'*

**mbingu** (mbingu) the sky.
*Nafikiri Mungu anakaa mbinguni.*

**mbio** (mbio) running fast.
*Abud alipiga mbio, akafika mbele yangu.*

**mbizi** (mbizi) diving into water.
*Nilipiga mbizi, nikaanza kuogelea.*

**mboga** (mboga) a vegetable.
*Napenda kula mboga kama hizi.*

**mbolea** (mbolea) fertilizer.
*Mkulima alinunua mbolea nzuri, magunia matatu.*

**mbona** why?
*Mbona umevunja kalamu hii?*

**mbu** (mbu) a mosquito—that is, a kind of small insect with wings which bites people and drinks their blood; people often get sick after it bites them.
*Pwani kuna mbu wengi.*

**mbunge** (wabunge) an MP—that is, someone who is chosen by people to be in the government.
*Raia wa huku walimchagua mbunge.*

**mbuyu** (mibuyu) a kind of big tree with a very thick trunk.
*Mbuyu ule ni mkubwa sana.*

**mbuzi** (mbuzi) a goat.
*Mbuzi huyu ananisumbua sana.*

**mbwa** (mbwa) a dog.
*Nampenda mbwa wangu.*

**mbweha** (mbweha) a jackal—that is, a kind of wild animal which looks like a small dog.
*Tazama mbweha wale wawili!*

**mchana** during the day.
*Watu hufanya kazi mchana na kulala usiku.*

**mchanga** sand.
*Maria anataka kucheza na mchanga ule, ufukoni.*

**mchango** (michango) gathering

together something.
*Watu wote walishirikiana katika mchango wa pesa.*

**mcheko** (micheko) laughing.
*Tulipomwona akivaa nguo za kigeni, tulishikwa na micheko.*

**mchele** (michele) rice.
*Mamangu alinunua mchele huu dukani.*

**mchezaji** (wachezaji) someone who plays a game.
*Wachezaji hawa hucheza mpira.*

**mchezo** (michezo) a game.
*Watoto hupenda kucheza michezo.*

**mchicha** (mchicha) spinach—that is, a kind of plant which has leaves that are good to eat.
*Mama anapika mchicha.*

**mchoro** (michoro) a drawing.
*Mwanafunzi alichora mchoro mkubwa ubaoni.*

**mchungwa** (michungwa) an orange tree.
*Michungwa kama hii huzaa machungwa makubwa.*

mbweha

**mchuzi** (michuzi) gravy; a kind of soup which is poured over rice.
*Watu wengi hula wali kwa mchuzi.*

**mchwa** (mchwa) termites—that is, small white insects which live together in holes in the ground.
*Malkia wa mchwa ni mkubwa kuliko wengine.*

**mdomo** (midomo) a mouth or a lip.
*Alitia njugu karanga mdomoni mwake.*

**mdudu** (wadudu) an insect or something like an insect; a little creature.
*Mdudu aliniuma jana usiku.*

**mea** to grow like a plant grows.
*Mihindi hii imemea vizuri.*

**Mei** (Mei) May.
*Mwezi wa Mei hufuata mwezi wa Aprili.*

**meko** the three stones which are used for cooking; the pot is put on them.
*Chombo kiko mekoni.*

**meli** (meli) a big boat or ship; a steamer.
*Nilipokwenda Mombasa niliona meli nyingi.*

**mende** (mende) a cockroach—that is, a kind of big insect.
*Niliona mende wengi chooni.*

**metameta** to sparkle.
*Jana usiku niliona nyota zikimetameta.*

**meya** (meya au mameya) a mayor—that is, someone who is the head of the government of a big town.
*Yule ni meya wa Nairobi.*

**meza** to swallow.
*Alimeza chakula kilichokuwa mdomoni mwake.*

**meza** (meza) a table.
*Kuna meza kubwa katika chumba cha kulia.*

**mfano** (mifano) sample or example—that is, something which you say or show to someone else to help him understand what you are talking about.
*Afrika ina miji mingi, kwa mfano: Nairobi, Accra, Kinshasa, na Monrovia.*

**mfanyi kazi** (wafanyi kazi) someone who works.
*Wafanyi kazi hujenga taifa.*

**mfereji** (mifereji) a water tap or a pipe which water goes through.
*Funga mfereji; maji haya yatosha.*

**mfugo** (mifugo) a herd or flock.
*Bwana Daudi ana mifugo mingi ya wanyama mbalimbali.*

**mfuko** (mifuko) a pocket or a purse or a bag.
*Alitia pesa katika mfuko wake.*

**mfululizo** (mifululizo) the going on and on of an action; the happening over and over of an action.
*Alinipiga mara tatu mfululizo.*

**mfupa** (mifupa) a bone.
*Samaki hii hailiki kwa sababu ya mifupa yake mingi.*

**mganga** (waganga) a kind of doctor.
*Babu yangu alikuwa mganga; alikuwa hutumia dawa ya aina mbalimbali katika kazi yake.*

**mgeni** (wageni) a visitor or someone from another place.
*Nilimkaribisha mgeni aingie nyumbani.*

**mgomba** (migomba) a banana tree.
*Migomba kama ile huzaa ndizi nyingi.*

**mgongo** (migongo) the back
*Mgongo wangu unaniuma sana.*

**mgonjwa** (wagonjwa) someone who is sick.
*Kuna wagonjwa wengi hospitalini.*

**mguu** (miguu) a leg.
*Meza hii ina miguu mitatu.*

**Mhindi** (Wahindi) an Indian—that is, someone from India.
*Wahindi ni watu wema.*

**mia** hundred.
*Watu mia tatu walihudhuria mkutano huo.*

**mila** (mila) custom; things which everyone does a certain way because that is the way to do it.
*Babu zetu walifuata mila za makabila yao.*

**milioni** a million; a thousand thousands.
*Elfu mara elfu ni milioni.*

**mimi** I; me.
*Mimi nitakwenda peke yangu.*

**minya** to squeeze.
*Usiminye ndizi hivyo!*

**miongoni mwa** among.
*Namwona Yusuf miongoni mwa wale wavulana. Niligundua kitabu changu miongoni mwa vitabu vyake.*

**mita** (mita) a metre—that is, a measure of how long something is; about a yard.
*Nguo hii ina urefu wa mita tatu.*

**miwani** (miwani) glasses or spectacles—that is, things made of glass which help people to see better.
*Siwezi kuona vizuri kwa sababu nimepoteza miwani yangu.*

**mja mzito** (waja wazito) a woman who is going to have a baby.
*Nilimbebea mja mzito sanduku yake.*

**mji** (miji) a city; a town.
*Nafikiri Kitale ni mji mzuri.*

**mjinga** (wajinga) someone foolish.
*Mjinga huyo alikula matope.*

**mjomba** (wajomba) uncle.
*Yule ni mjomba wangu.*

**mjukuu** (wajukuu) a grandchild.
*Mzee huyo ana wajukuu wengi.*

**mjumbe** (wajumbe) an MP—someone who is chosen by people to be in the government; someone who is sent to do something.
*Raia wa huku walimchagua mjumbe.*

**mkahawa** (mikahawa) a restaurant—that is, a place where people go to eat food and drink coffee.
*Tuliingia mkahawani, tukanywa kahawa.*

**mkasi** (mikasi) scissors.
*Alikata karatasi kwa kutumia mkasi.*

**mkate** (mikate) a loaf of bread; a loaf of anything else.
*Mamangu alikwenda dukani, akanunua siagi na mikate miwili.*

**mke** (wake) a wife.
*Huyu ni Yohana na yule ni mke wake. Niliwakuta wageni pamoja na wake zao.*

**mkebe** (mikebe) a tin.
*Mkebe huu una maharagwe ndani yake.*

**mkeka** (mikeka) a mat or rug.
*Mkeka huu ni mzuri kuliko ule.*

**mkewe** (wakeze) his wife.
Huyu ni Yohana na yule ni *mkewe.*

**mkia** (mikia) a tail.
*Kondoo wangu ana mkia mpana.*

**mkoloni** (wakoloni) a colonial—that is, someone who leaves his own country, settles in another country, and then tries to help the government of his own country to rule the country he has settled in.
*Tuwafukuze wakoloni wote kutoka katika Afrika. Kenya ilitawaliwa na wakoloni waliotoka Uingereza kabla hawajafukuzwa na wananchi.*

**mkono** (mikono) someone's hand or arm.
*Mwanafunzi aliinua mkono wake wa kulia.*

**mkopo** (mikopo) a loan—that is, something, such as money, which someone lends to someone else.
*Hakuwa na pesa za kutosha, akapata mkopo benkini.*

**mkubwa** (wakubwa) a leader.
*Rais wa nchi yetu ndiye mkubwa wetu.*

**mkuki** (mikuki) a spear—that is, a long, wooden stick with a pointed end made of metal.
*Nilipoingia ndani ya muziamu niliona mikuki mingi na ngao nyingi.*

**mkuki**



**mkulima** (wakulima) a farmer; someone who has a farm or works on a farm.
*Mkulima yule amefanya kazi nyingi leo.*

**mkutano** (mikutano) a group of people meeting together.
*Watu wengi walihudhuria mkutano huo.*

**mkuyu** (mikuyu) a kind of big tree; its fruit, which is called a wild fig, is good to eat.
*Kweli mkuyu ule ni mti mkubwa sana.*

**mlafi** (walafi) someone who eats too much.
*Mlafi huyo amekula chakula chote.*
**mlango** (milango) a door.
*Mlango ule u wazi.*
**mle** over there, inside.
*Nafikiri yumo mle shimoni.*
**mlima** (milima) a mountain.
*Mlima wa Kenya ni mrefu sana.*
**mlinzi** (walinzi) a guard.
*Mlinzi huyu hulinda nyumba yetu.*
**mmea** (mimea) a plant.
*Mimea hii mikubwa ina maua mazuri.*
**mnazi** (minazi) a kind of palm tree; a big, hard fruit called a coconut grows on it.
*Minazi kama ile huzaa nazi kubwa.*
**mno** too much.
*Siwezi kuendelea; nimechoka mno.*
**mnofu** (minofu) meat without any bones in it.
*Hamisi hataki mifupa; atakula minofu tu.*
**mnunuzi** (wanunuzi) a customer.
*Mwuzaji alimwonyesha mnunuzi mboga za aina mbalimbali.*
**mnyama** (wanyama) an animal.
*Napenda kuwawinda wanyama.*
**-mo** is inside there; are inside there.
*Pesa zimo mfukoni. Vitabu vimo humu ndani ya sanduku. Mnyama yumo mle shimoni.*
**-moja** one.
*Nataka kitabu kimoja. Niletee kalamu moja. Mgeni mmoja amefika.*
**moshi** (mioshi) smoke or steam.
*Moto ule unatoa moshi mwingi.*
**moto** (mioto) fire; being hot.
*Mama aliuzima moto huo.*
**motokaa** (motokaa) an automobile; a car.
*Kama ningekuwa na pesa ningenunua motokaa nzuri.*
**moyo** (mioyo) a heart.
*Nasikia moyo wangu ukipigapiga. Kitendo cha shujaa huyo kilinitia moyo.*
**mpaka** (mipaka) boundary or border; the line where one country meets another country.
*Ramani hii yaonyesha mipaka ya Kenya.*

mnazi



17

**mpaka** until; up to.
*Alihesabu kutoka moja mpaka kumi. Tutasafiri kutoka Nairobi mpaka Mombasa. Tulizungumza mpaka kukawa usiku.*

**mpamba** (mipamba) a cotton plant.
*Mipamba huzaa pamba.*

**mpango** (mipango) a plan.
*Mpango wangu mzuri kuliko wako.*

**mpelelezi** (wapelelezi) someone who finds out secrets.
*Mpelelezi aligundua habari hii.*

**mpenzi** (wapenzi) someone who is loved by someone else.
*Huyu ni mpenzi wangu.*

**mpira** (mipira) a football.
*Nilinunua mpira mpya tucheze nao.*

**mpira** (mipira) the tube of a tyre.
*Mpira huu umetoboka.*

**mpishi** (wapishi) a cook.
*Mpishi hupika chakula. Huyu ni mpishi mzuri sana; jina lake Mwaura.*

**mpunga** (mipunga) a rice plant; rice that has just been gathered.
*Ni nani aliyepanda mipunga hii?*

**mraba** (miraba) a square or something like a square.
*Chora mraba mkubwa ubaoni.*

**mrembo** (warembo) a girl who is dressed up and looks pretty.
*Mrembo huyu amejipamba sana.*

**msaada** (misaada) help.
*Maskini alipokea msaada wa pesa.*

**msafara** (misafara) a caravan—that is, a group of animals or things moving in a line.
*Siafu walikuwa katika msafara mnene.*

**msafiri** (wasafiri) someone who travels from place to place.
*Wasafiri wale walinisaidia.*

**msalani** in the lavatory.
*Amekwenda msalani.*

**msamiati** (misamiati) a list of words.
*Maneno yote yameandikwa kwenye msamiati.*

**msemo** (misemo) a saying—that is, something which is said many times by people.
*Kuna msemo usemao, 'Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.'*

**mshahara** (mishahara) wages; money which someone is paid for doing work.
*Nataka mshahara wangu uongezeke.*

**mshale** (mishale) an arrow—that is, a short, wooden stick with a pointed end made of metal or stone; a bow is used to make it fly through the air.
*Mwindaji ana uta na mishale minne.*

mshale



**mshindani** (washindani) someone who is trying to win in a competition.
*Washindani wale wanakimbia sana.*

**mshindi** (washindi) a winner.
*Katika mashindano hayo ni Yohana aliyekuwa mshindi.*

**mshipi** (mishipi) a belt.
*Mvulana amevaa suruali na mshipi.*

**msichana** (wasichana) a young girl.
*Kuna wasichana wanne uwanjani.*

**msikiti** (misikiti) a mosque—that is, a kind of church, used by people who believe that the One who made the world sent Mohammed as His messenger.
*Twende msikitini.*

**msingi** (misingi) a foundation.
*Kabla ya kujenga jengo ni lazima kuweka msingi.*

**msitu** (misitu) a forest of small trees, such as thorn trees, and bushes.
*Twiga hukaa msituni.*

**msozi** (msozi) a sun-bird—that is, a kind of small, brightly coloured bird that drinks honey from flowers.
*Msozi yule ana rangi ya kupendeza.*

**mstari** (mistari) a line.
*Chora mstari mrefu ubaoni.*

**msumari** (misumari) a nail.
*Niletee nyundo na misumari minne.*

**msumeno** (misumeno) a saw.
*Ukitaka kufanya kazi ya useremala, lazima uwe na nyundo, misumari, msumeno, na vifaa vingine kama hivyo.*

**mswaki** (miswaki) a little brush for cleaning your teeth.
*Alisafisha meno yake kwa kutumia mswaki huo.*

**mtaa** (mitaa) part of a town.
*Amin hukaa katika mtaa wa Waesia.*

**mtaalamu** (wataalamu) someone who has learned many things.
*Mwalimu wetu ni mtaalamu.*

**mtalii** (watalii) a tourist—that is, someone who travels to a different country to see it.
*Kuna watalii wengi katika basi hilo.*

**mtama** (mitama) millet; a kind of grain.
*Mama alinunua mtama nusu kilo.*

**mtambo** (mitambo) a kind of machine, especially a machine with a spring in it.
*Mtambo huu wa saa umeharibika.*

**mtego** (mitego) a trap.
*Ni nani aliyetega mtego huu?*

**mtelemko** (mitelemko) a place where the ground goes down.
*Kwenye ukingo wa mto kulikuwa na mtelemko mrefu.*

**mti** (miti) a tree; wood.
*Mti ule mkubwa sana.*

**mtihani** (mitihani) a test.
*Nilijaribu mtihani, nikafaulu.*

**mto** (mito) a river.
*Mto wa Tana ni mpana.*

**mto** (mito) a pillow.
*Paka alilala juu ya mto.*

**mtondo** the third day after today.
*Tutakwenda kesho kutwa na kurudi mtondo.*

**mtondo goo** the fourth day after today.
*Tusipoweza kurudi mtondo, tutarudi mtondo goo.*

**mtoto** (watoto) a child.
*Mwanamke huyu ana watoto wawili.*

**mtu** (watu) a man or woman.
*Watu wengi huishi huku.*

**mtumbwi** (mitumbwi) a canoe—that is, a kind of small boat.
*Mimi naogopa kusafiri baharini kwa mtumbwi mdogo kama huu wako.*

**mtumishi** (watumishi) a servant.
*Tajiri yule aliajiri watumishi wengi.*

**mtumwa** (watumwa) a slave.
*Kila mtumwa hutamani uhuru.*

**mtungi** (mitungi) a clay pitcher—that is, a kind of jug that water is kept in.
*Mtungi ulianguka, ukavunjika.*

**mtunza** (watunza) someone who cares for or protects something else or someone else.
*Yaya ni mtunza watoto.*

**muda** some time; a space of time.
*Nimekaa hapa Nairobi kwa muda wa miaka mitatu.*

**muhimu** important.
*Kazi hii ni muhimu. Haya ni mambo muhimu.*

**muhogo** (mihogo) a cassava plant—that is, a kind of plant that has roots which are good to eat.

*Ni nani aliyepanda muhogo huu? Watu wengi hupenda kula muhogo.*

**mulika** to shine.
*Nyota nyingi sana zamulika usiku.*

**mume** (waume) a husband.
*Niliwaona Hadija na mume wake.*

**mundu** (miundu) a sickle—that is, a kind of big, curved knife.
*Mundu huu ni mkali sana.*

**Mungu** (miungu) the One who made the world; God; Allah.
*Tulimwomba Mungu atusaidie.*

**muwa** (miwa) sugar cane—that is, a kind of plant which has sugar in its stem.
*Watoto hupenda kula miwa.*

**muziamu** (muziamu) a museum.
*Nairobi kuna muziamu nzuri sana.*

**muziki** (muziki) music.
*Huyu ni mpiga muziki katika bendi.*

**mvi** (mvi) grey hair.
*Mzee yule ana mvi.*

**mviringo** (miviringo) a circle.
*Mwalimu alichora mviringo mkubwa ubaoni.*

**mvivu** (wavivu) someone who is very lazy; a lazybones.
*Amka mvivu na kufanya kazi yako!*

**mvua** (mvua) rain.
*Mvua inanyesha sana.*

**mvulana** (wavulana) a young man.
*Wachezaji wote ni wavulana.*

**mvuvi** (wavuvi) a fisherman.
*Kazi ya mvuvi ni kuvua samaki.*

**Mwafrika** (Waafrika) someone who is from Africa.
*Mimi ni Mwafrika.*

**mwaga** to spill something, such as water.
*Ni nani aliyemwaga maziwa haya?*

**mwagia** to spill something into or onto something else.
*Mtoto aliimwagia karatasi rangi.*

**mwagika** to be spilled.
*Maziwa yote yamemwagika.*

**mwaka** (miaka) a year.
*Mwalimu wetu alizaliwa mwaka wa 1940.*

**mwaliko** (mialiko) a loud snap or clap.
*Je, ulisikia mwaliko huo?*

**mwalimu** (walimu) a teacher.
*Sisi twampenda mwalimu wetu.*

**mwana** (wana) a son or daughter.
*Kila mwanamke huwapenda wanawe.*

**mwanachama** (wanachama) a member of a club or association—that is, someone who belongs to a group of people who like to do things together.
*Wanachama wote walikwenda pwani.*

**mwanafunzi** (wanafunzi) a student—that is, someone who studies in a school.
*Wanafunzi hawa wamekwisha jifunza kusoma na kuandika.*

**mwanamke** (wanawake) a woman.
*Amina ni mwanamke mfupi.*

**mwanamume** (wanaume) a man.
*Ali ni mwanamume mrefu.*

**mwananchi** (wananchi) someone who belongs to a certain country.
*Sisi sote ni wananchi.*

**mwanangu** (wanangu) my son or daughter.
*Mwanamke alimwita mtoto wake mwanangu.*

**mwanasesere** (wanasesere) a child's doll.
*Mtoto anapenda mwanasesere wake.*

**mwanasheria** (wanasheria) a lawyer—that is, someone who knows the law very well and whose work is to explain the law.

*Mwanasheria huwa na elimu nyingi.*

**mwandazi** (waandazi) someone whose work is to get a table ready for a meal.
*Maria anafanya kazi kama mwandazi katika mkahawa huo.*

**mwanga** (mianga) light.
*Naweza kuona vizuri kwa sababu ya mwanga wa jua.*

**mwangaza** (miangaza) light; a hole that lets in light.
*Nilimwona chui kwa mwangaza wa tochi. Chumbani mna giza tupu; hamna mwangaza wo wote.*

**mwanzo** (mianzo) beginning.
*Mwanzo wa mwaka huwa ni mwezi wa Januari.*

**Mwarabu** (Waarabu) an Arab; someone from a country which is named Arabia.
*Waarabu wengi husafiri kwa ngamia.*

**mwashi** (waashi) a mason—that is, someone whose work is to build things using stones or bricks.
*Baba yangu ni mwashi mzuri sana.*

**Mwasia** (Waasia) an Asian; someone from Asia.
*Mwasia huyo anauza motokaa yake.*

**mwembe** (miembe) a mango tree.
*Mwembe ule ni mkubwa sana.*

**mwendo** (miendo) going.
*Gari limeshika mwendo vizuri.*

**mwenendo** (mienendo) going on, especially a way of behaving that is going on.
*Watu hawa wana mienendo myema.*

**mwenyeji** (wenyeji) the owner of a house; someone who belongs to a certain place and is not a stranger there.
*Mwenye nyumba huitwa mwenyeji. Watu hawa si wageni; ni wenyeji.*

**mwenyekiti** (wenyekiti) a chairman—that is, someone who is in charge when a group of people are meeting together.
*Hamisi alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa mkutano huo.*

**mwenzi** (wenzi) a friend.
*Huyu ndiye mwenzi wangu.*

**Mwesia** (Waesia) an Asian; someone from Asia.
*Joginder ni Mwesia, naye mtu mwema.*

**mwezi** (miezi) the moon; a moon.
*Dunia yetu ina mwezi mmoja.*

**mwezi** (miezi) a month.
*Mwezi wa Septemba una siku thelathini.*

**mwewe** (mwewe) a hawk—that is, a kind of big bird which eats chickens.
*Mwewe amemnyakua kifaranga.*

**mwiba** (miiba) a thorn.
*Yohana alichomwa na mwiba huu.*

**mwiko** (miiko) a trowel—that is, something like a big spoon.
*Nipe mwiko huo.*

**mwili** (miili) a body.
*Mwili wake ni mnene kidogo.*

**mwimbaji** (waimbaji) someone who sings.
*Mwimbaji huyu huimba vizuri.*

**mwindaji** (wawindaji) someone who hunts animals or birds.
*Mwindaji yule alipata swala wawili.*

**mwisho** (miisho) end.
*Desemba ni mwezi wa mwisho wa mwaka.*

**mwishowe** as the last thing done.
*Tulimaliza kazi zote na mwishowe tukarudi nyumbani.*

**mwitu** (miitu) a forest of large trees.
*Chui amejificha mwituni.*

**mwivi** (wevi) a thief.
*Askari polisi alimkamata mwivi.*

**mwizi** (wezi) a thief.
*Askari polisi alimkamata mwizi.*
**mwota ndoto** (waota ndoto) someone who dreams often.
*Mwota-ndoto huota ndoto usingizini.*
**mwungwana** (waungwana) a gentleman; someone who is polite and kind.
*Nampenda sana kwa sababu ni mwungwana.*
**mwuzaji** (wauzaji) someone who sells things.
*Mwuzaji yule huuza chakula.*
**mzazi** (wazazi) a mother or father.
*Niliwaona watoto pamoja na wazazi wao.*
**mzee** (wazee) someone who is old.
*Wazee hutembea polepole.*
**mzigo** (mizigo) a load—that is, something which someone carries.
*Mzigo huu ni mzito kuliko huo.*
**mzinga** (mizinga) something like a long, empty barrel which people hang in a tree so bees will live in it.
*Mna asali nyingi ndani ya mzinga ule.*
**mzungu** (wazungu) a European—that is, someone who is a white colour and is from a place named Europe.
*Yeye ni mzungu.*

# n

**na** and; with; has or have.
*Nilichukua kalamu na karatasi.*
*Maria alikwenda na Yohana.*
*Ninacho kitabu chako. Paulo ana pesa nyingi.*
**nafaka** (nafaka) grain.
*Ngano ni namna ya nafaka.*
**nafasi** (nafasi) an opportunity or chance; space or room.
*Nilitaka kwenda mjini lakini sikuwa na nafasi. Basi hili limejaa watu; hakuna nafasi ya mtu mwingine.*
**namba** (nambo) a number.
*Kila motokaa ina namba yake.*
**namna** (namna) a kind or sort.
*Sipendi nguo ya namna hii.*
**nanasi** (mananasi) a pineapple.
*Mamangu alinunua mananasi mawili sokoni.*

**nanasi**

**-nane** eight.
*Watu wanane watakuja. Niletee vijiko vinane. Nataka kalamu nane. Soma somo la nane. Alihesabu moja mpaka nane.*
**nani** who?
*Nani huyu? Hawa ni nani?*
**nawa** to wash your hands.
*Roda amenawa mikono yake.*
**nazi** (nazi) a coconut—that is, a kind of big, hard fruit which grows on palm trees near the sea.
*Mamangu alinunua nazi hizi tatu sokoni.*
**nchi** (nchi) a country.

*Paulo alisafiri katika nchi za ugenini.*

**ndama** (ndama) a calf; a young cow.
*Ndama yule ni mdogo.*

**ndani** inside.
*Ndani ya pango mna giza. Njoo humu ndani.*

**ndefu** (tazama -refu)

**ndege** (ndege) a bird.
*Ndege hawa huitwa njiwa.*

**ndege** (ndege) an aeroplane.
*Hatujapata nafasi ya kusafiri kwa ndege.*

**ndi-** this is indeed; that is indeed.
*Hiki ndicho kitabu changu. Wale ndio wevi. Kalamu zangu ndizo hizo. Yeye ndiye mjinga niliyemtaja!*

**ndimu** (ndimu) a lime—that is, a kind of fruit like a little green orange which tastes sour.
*Mama amenunua ndimu nyingi.*

**ndiyo** yes, that is so.
*Nilimwuliza kama ana pesa, akasema, 'Ndiyo, bwana.'*

**ndizi** (ndizi) a banana.
*Ndizi hizi zimeoza.*

**ndoa** (ndoa) a wedding—that is, the ceremony when someone is married to someone else.
*Amina na Yusuf walioana nami nilihudhuria ndoa.*

**ndoana** (ndoana) a fish-hook.
*Juma alinunua ndoana tatu kwa sababu alitaka kuvua samaki mtoni.*

**ndoo** (ndoo) a bucket.
*Ndoo ina maji.*

**ndoto** (ndoto) a dream.
*Mimi huota ndoto za kupendeza.*

**ndovu** (ndovu) an elephant.
*Ndovu ni mnyama mkubwa sana. Nilimwona ndovu akiyala majani ya mti ule.*

**ndugu** (ndugu) a relative.
*Alimkuta Abud pamoja na ndugu zake watatu.*

**neema** (neema) grace—that is, help from God.
*Mungu alitupa sisi neema nyingi.*

**nenda** go!
*Nenda nje!*

**-nene** fat or thick.
*Mtoto huyo ni mnene sana. Niletee kamba ile nene.*

**nenepa** to get fat.
*Paulo amenenepa sana.*

**neno** (maneno) a word.
*Sipendi watu wasemao maneno mengi.*

**ng'aa** to be shining.
*Jua linang'aa sana.*

**ngalawa** (ngalawa) an outrigger canoe—that is, a kind of small boat with pieces of wood fixed to it so that it cannot turn over easily.
*Ngalawa haiwezi kupinduka kama mtumbwi.*

**-ngali** still.
*Wazazi wako wangali hai? Kitabu kingali kichafu? Ingali inanyesha. Tulikuwa tungali kufanya kazi.*

**ng'ambo** (ng'ambo) the other side, especially of a river.
*Tulivuka mto tukapumzika kwenye ng'ambo ya pili.*

**ngamia** (ngamia) a camel.
*Kuna ngamia watatu kule.*

**ngano** (ngano) wheat; a kind of grain.
*Ukisaga ngano utapata unga.*

**ngao** (ngao) a shield—that is, a thing someone uses to protect himself from other things which are thrown at him.
*Ngao hii ni ndefu.*

**-ngapi** how many?
*Kuna watu wangapi? Kuna viti vingapi? Ulipanda mbegu ngapi?*

**ngazi** (ngazi) a ladder or some steps.
*Nilipanda ngazi nikafika juu ya ukuta.*

ngano

ngao



**nge** (nge) a scorpion—that is, a creature like a big insect that can sting with its tail.
*Huku kuna nge wengi.*

**ng'oa** to dig something out; to pull a plant out of the ground.
*Nitang'oa magugu haya yote.*
*Daktari aling'oa jino langu baya.*

**ngoja** to wait.
*Ngoja kidogo; nitarudi baada ya dakika chache.*

**ngojea** to wait for something or someone.
*Tulisimama tukimngojea Rais.*

**ngoma** (ngoma) a drum.
*Mtoto anapiga ngoma yake.*

**ngoma** (ngoma) a dance.
*Tuliwatazama watu wakicheza ngoma za kienyeji.*

**ng'ombe** (ng'ombe) a cow.
*Ng'ombe hawa hutoa maziwa mengi.*

**ngozi** (ngozi) leather; the outside part of an animal's body.
*Hamisi alichuna ngozi ya kondoo.*

**ngumi** (ngumi) a fist—that is, a closed hand.
*Salim alinipiga ngumi.*

**nguo** (nguo) cloth; a dress.
*Hadija amenunua nguo mpya.*

**nguruma** to growl or to roar.
*Naogopa nisikiapo simba wakinguruma.*

**ngurumo** (ngurumo) a growl or roar.
*Tuliposikia ngurumo ya simba, tuliogopa.*

**nguruwe** (nguruwe) a pig—that is, a kind of fat animal.
(See picture on page 54)
*Nguruwe wa mwitu anakula mahindi yangu.*

nguruwe

**nguvu** (nguvu) force or power or being strong.
*Askari alibisha mlango kwa nguvu.*

**ni** is; are; am.
*Hiki ni kitabu. Yale ni matunda yangu. Mimi ni mjinga.*

**nia** (nia) intention; aim.
*Nia ya Serikali ni kuwapatia watu wote kazi nzuri yenye maana.*

**ning'inia** to swing.
*Tulifunga majani kwa kamba, yakaning'inia juu ya mbuzi.*

**nini** what?
*Nini hii? Ulisema nini?*

**ninyi** you all.
*Ninyi mtakwenda peke yenu.*

**njaa** (njaa) hunger; being hungry.
*Nilimpa chakula kwa sababu alikuwa na njaa.*

**nje** outside.
*Mpira ulibingirika nje ya kabati. Nendeni nje.*

**njema** (tazama -ema)

**njia** (njia) a path or way.
*Tufuate njia hii.*

**njia-panda** (njia-panda) a place where one road or path splits into two.
*Alipofika kwenye njia-panda hakujua ni njia ipi iliyoelekea mjini.*

**njiwa** (njiwa) a dove—that is, a kind of bird.
*Nyama ya njiwa ni tamu. Angalia njiwa wale.*

**njoo** come!
*Njoo hapa.*

**njugu-karanga** (njugu-karanga) a ground-nut—that is, a kind of seed which grows under the ground and which is good to eat.
*Watoto hupenda kula njugu-karanga.*

njugu-karanga

**-nne** four.
*Nataka kalamu nne. Wavulana wanne watakwenda. Ninunulie vitabu vinne. Alisoma somo la nne.*

**nona** to get fat.
*Ng'ombe zangu wamenona vizuri.*

**-nono** fat.
*Ng'ombe hawa ni wanono. Nitanunua mbuzi yule mnono. Yeye anapata mshahara mnono.*

**noti** (noti) a note.
*Juma alimpa noti ya shilingi tano.*

njiwa

**Novemba** (Novemba) November.
*Mwezi wa Novemba hufuata mwezi wa Oktoba.*
**nuka** to smell bad.
*Chakula hiki kibaya; kinanuka fee.*
**nukia** to smell good.
*Maua haya yananukia vizuri.*
**nukta** (nukta) a second.
*Kila dakika ina nukta sitini.*
**nung'unika** to grumble.
*Mfanyi kazi hakupenda kazi yake, akaanza kunung'unika.*
**nunua** to buy.
*Nilinunua baiskeli hii jana.*
**nunulia** to buy something for someone.
*Alimnunulia mama yake kitabu kipya.*
**nusa** to smell something.
*Mbwa wangu ananusa mbwa wako.*
**nusu** (nusu) a half.
*Tunataka nusu ya mkate huu.*
**nusura** almost.
*Alikuwa nusura afe. Aliwapiga nusura kuwaua.*
**nya** to discharge—that is, to let something out, as from the body.
*Mtoto mchanga amekunya mavi.*
**nyakua** to snatch; to catch something suddenly.
*Mwivi alinyakua mfuko wa Hadija.*
**nyama** (nyama) meat.
*Nimekula nyama ya kuku.*
**nyamaza** to be silent.
*Nataka watoto wote wanyamaze kimya.*
**nyang'anya** to take something from someone when he does not want you to have it; to steal.
*Huyo alininyang'anya pesa zangu!*
**nyani** (nyani) a baboon.
*Nyani huyo ni mkubwa sana.*
**nyanya** (nyanya) a tomato—that is a kind of red fruit which grows on a small plant.
*Nyanya hizi ni tamu.*
**nyanya** (nyanya) a grandmother.
*Nyanya yangu ana umri wa miaka sabini hivi.*
**nyati** (nyati) a buffalo—that is, a big wild animal like a cow which lives in the forest.
*Nilipowaona nyati nilikimbia.*

nyati

**nyesha** to rain.
*Mvua inanyesha. Kutanyesha kesho.*
**nyoa** to shave—that is, to cut off hair with a kind of knife called a razor.
*Baba yangu hunyoa kila asubuhi.*
**nyoka** (nyoka) a snake.
*Nyoka hawana mikono wala miguu.*
**nyonga** to squeeze or twist the neck of someone or of some anima.
*Kwa kahati mbaya kamba ilimshika shingoni, ikamnyonga.*

**nyonya** to suck.
*Mtoto mchanga alinyonya apate maziwa.*
**nyosha** to make something straight.
*Mtoto alinyosha mkono wake kushika ndizi.*
**nyota** (nyota) a star—that is, one of the tiny lights which are seen in the sky at night; they are other suns which are very far away.
*Zile ni nyota; angalia jinsi zinavyometameta.*
**nyuki** (nyuki) a bee.
*Nyuki waliniuma nilipojaribu kupata asali.*
**nyuma** (nyuma) behind.
*Alinisukuma nyuma.*
*Wamejificha nyuma ya miti ile.*
**nyumba** (nyumba) a house.
*Nyumba yake ina vyumba vitatu.*
**nyundo** (nyundo) a hammer.
*Baba yangu alichukua nyundo yake, akaenda kutafuta misumari.*
**nywa** to drink.
*Utakunywa soda hii.*
*Hatujanywa hata kidogo.*
**nzi** (nzi) a fly.
*Nzi huleta uchafu; wafukuze!*
**nzige** (nzige) a locust—that is, a kind of insect like a big grasshopper; they often travel in large groups.
*Nzige walifika kwa wingi, wakala ngano yote.*

## O

**oa** to marry a wife.
*Hamisi alimwoa Anna.*
**oga** to wash yourself; to take a bath.
*Watoto wanaoga sasa.*
**-oga** afraid.
*Nafikiri huyu ni mtu mwoga.*
*Sipendi wasichana waoga kama wewe.*
**ogelea** to swim.
*Yeye hatakufa maji kwa sababu anajua kuogelea.*
**ogopa** to be afraid.
*Wasichana huogopa nyoka.*
**okoa** to save someone.
*Mtoto alianguka baharini, nikamwokoa.*
**okota** to pick up something.
*Niliona shilingi njiani, nikaiokota.*
Oktoba (Oktoba) October.
*Mwezi wa Oktoba hufuata mwezi wa Septemba.*
**olewa** to be married by a husband.
*Anna aliolewa na Hamisi.*
**omba** to ask for; to beg.
*Watoto walimwomba mama yao ruhusa ya kwenda nje.*
**ona** to see; to think; to feel.
*Unaweza kuona nyumba ile?*
*Naona kitu hiki ni kidogo. Waonaje?*
**onana** to see each other.
*Tulionana na Hamisi. Kwa heri ya kuonana.*
**ondoa** to take something away.
*Ondoeni sahani hizi chafu!*
**ondoka** to leave; to begin a trip or safari.
*Wasafiri waliondoka kabla ya saa moja ya asubuhi.*
**onea** to behave badly toward someone.
*Mtoto huyu mkorofi anawaonea watoto wale wengine.*
**onekana** to be able to be seen.
*Kaa wengi huonekana pwani.*
**ongea** to talk.
*Sisi tumeongea kwa muda mrefu.*
**ongeza** to increase—that is, to make more; to make bigger.
*Nitaongeza mshahara wako.*
**ongezeka** to be increased—that is, to be made more; to be made

bigger.
*Twataka fahari ya nchi yetu iongezeke.*
**ongoza** to lead.
*Kazi ya kiongozi ni kuongoza.*
**onya** to warn—that is, to tell someone that he should be careful not to do something.
*Mzazi aliwaonya watoto wasicheze barabarani.*
**onyesha** to show.
*Amenionyesha motokaa yake mpya.*
**-o -ote** any at all.
*Sitaki tunda lo lote. Sijawaona watu wo wote. Sina pesa zo zote. Hana mahindi yo yote.*
**orodha** (orodha) a list.
*Aliandika majina yote katika orodha hii.*
**-ororo** smooth or soft.
*Nyama hii ni nyororo. Rinda lake ni jororo. Nataka kipande chororo cha nyama. Maembe haya ni mororo.*
**osha** to wash.
*Baiskeli yake ni chafu; ataiosha kesho.*
**ota** to sprout—that is, to grow like a plant; to start to grow like a plant.
*Mimea yote inaota. Mbegu hizi zitaota vizuri.*
**ota** to dream.
*Je, uliota ndoto usiku uliopita?*
**ota** to sit in the sun or near a fire.
*Wazee hao wahaota jua.*
**-ote** all; all of something.
*Nimepoteza pesa zote. Tumekula chakula chote. Sisi sote tutakwenda. Ninyi nyote mtanisaidia.*
**ovyo** in a very careless way.
*Mvivu aliweka vitu vyake ovyo.*
**oza** to be bad; to be spoiled.
*Maembe haya yameoza; siwezi kuyala.*

# p

**pa** to give to someone.
*Amenipa zawadi. Nitakupa pesa.*
**paa** to go up.
*Tiara yangu inapaa juu kwa juu.*
**paa** (paa) an antelope or buck.
*Paa wale wanakimbia sana.*
**paa** (mapaa) a roof.
*Paa lile ni la makuti.*
**paaza** to make something go up.
*Usipaaze sauti yako!*
**paka** to paint on; to spread something, like mud, on something else.
*Kesho nitapaka nyumba yangu rangi.*
**paka** (paka) a cat.
*Nampenda paka wangu sana.*
**pakacha** (mapakacha) a kind of little basket.
*Nipe pakacha hilo la maembe.*
**pakia** to put something into a boat or onto a train or bus.
*Tulipakia mizigo yetu katika gari la moshi.*
**pakua** to give out food; to dish out food.
*Maria alinisaidia kupakua chakula.*
**pale** over there.
*Nenda pale.*
**pamba** to decorate—that is, to make something or someone look pretty.
*Maria alimpamba dada yake kwa mapambo mazuri.*
**pamba** (pamba) cotton.
*Dada yako hununua nguo za pamba.*
**pambanua** to see or tell how one thing is different from another thing.
*Unaweza kupambanua vitabu hivi?*
**pambazuka** to be the start of day; to be morning when the sun has risen.

*Kumepambazuka.*

**pambo** (mapambo) a decoration—that is, something which makes something else look pretty.
*Maua haya ya rangi ni pambo la rinda hili.*

**pamoja** together.
*Twende pamoja. Nilikwenda pamoja na rafiki zangu.*

**-pana** wide or flat.
*Barabara hii ni pana. Hiki ni kitanda kipana. Mkeka huu ni mpana.*

**pancha** (pancha) a puncture.
*Mpira wa baiskeli yangu una pancha.*

**panda** to go up; to climb.
*Wote walipanda mlima wa Suswa.*

**panda** to plant a seed or small plant.
*Kesho tutapanda mbegu hizi zote.*

**panga** to put something in order.
*Amepanga vitabu hivi vizuri.*

**panga** to rent—that is, to pay money so that you can use something for a while.
*Tumepanga nyumba hii mpya.*

**panga** (mapanga) a kind of big knife or sword which is used to cut down bushes and small trees.
*Panga langu ni kali kuliko lako.*

**pango** (mapango) a cave or hole.
*Mnyama aliingia katika pango lile.*

**pangusa** to sweep or to dust.
*Pangusa vumbi, tafadhali.*

**panya** (panya) a mouse or rat.
*Paka akiondoka, panya hutawala.*

**panzi** (panzi) a grasshopper.
*Panzi kama huyu huweza kuruka juu sana.*

**papa** (papa) a shark—that is, a kind of big fish with lots of teeth.
*Watu wanaoogelea huogopa papa.*

panzi

**papai** (mapapai) a pawpaw—that is, a kind of large, sweet fruit.
*Mamangu amenunua mapapai mawili.*

mapapai

**papasa** to rub something gently with your hand.
*Unaweza kumpapasa mbwa wangu.*

**papasi** (mapapasi) a tick—that is, a kind of little insect that sucks blood.
*Nina papasi mguuni.*

**pasi** (pasi au mapasi) an iron—that is, a thing of hot metal that is pushed over clothes to make them dry and flat.
*Dobi hujua kupiga pasi.*

**pasua** to tear.
*Nitapasua karatasi hizi.*

**pasuka** to be torn.
*Nguo hii imepasuka vibaya.*

**pata** to get.
*Nilipata shilingi tatu jana.*
*Nitakwenda nipate kuona.*

**patia** to get something for someone.
*Nitakupatia kisu kikali.*

**pazia** (mapazia) a curtain.
*Juma, telemsha mapazia yote.*

**peke** (peke) being alone.
*Nataka kwenda peke yangu.*

**pekee** being alone.
*Huyo ni mtu wa pekee.*

**peleka** to send; to take.
*Walipeleka matunda sokoni.*

**pelekea** to send something to someone.
*Nitampelekea Hamisi zawadi.*

**pembe** (pembe) an animal's horn; ivory.
*Pembe za swala yule ni ndefu.*

**pembe** (pembe) a corner.
*Mtoto alisimama pembeni mwa chumba.*

**pembea** to swing.
*Mkia wa twiga ulipembea huku na huko.*

**penda** to like or to love.
*Nawapenda wazazi wangu sana.*

**pendeza** to be pleasing; to make someone like something.
*Alituimbia wimbo wa kupendeza.*

**pepea** to wave in the air.
*Bendera ile inapepea sana.*

**pepeta** to winnow—that is, to throw grain up in the air and catch it again, so that the leaves and grass and soil all blow away.
*Nafikiri kupepeta ni kazi ngumu.*

**pepo** (pepo) a spirit—that is, someone without a body, like a fairy or genie.
*Babangu aliniambia kuwa kuna pepo wema na pepo wabaya.*

**pera** (mapera) a guava—that is, a kind of small, green fruit with lots of seeds in it.
*Mtoto alikula mapera manne.*

**peremende** (peremende au maperemende) sweets.
*Watoto hupenda kula peremende.*

**pesa** (pesa) money.
*Mwivi aliiba pesa zangu.*

**pete** (pete) a ring.
*Pete hii ni ya dhahabu.*

**petroli** (petroli) petrol.
*Motokaa yako ina haja ya petroli.*

**pewa** to be given something.
*Nimepewa zawadi na Yohana.*

**-pi** which?
*Unataka kitabu kipi? Ulimwona mtoto yupi? Utanunua mapera yapi? Ulipasua karatasi zipi?*

**pia** altogether.
*Wote walikwenda, wavulana na wasichana pia.*

**picha** (picha) a picture or photograph.
*Kitabu hiki kina picha nzuri sana.*

**piga** to hit.
*Alimpiga mbwa kwa fimbo.*

**pigana** to fight; to hit each other.
*Watoto wale wanapigana.*

**pigania** to fight for something; to hit someone in order to get something.
*Wazazi wetu walipigania uhuru wa Kenya.*

**pika** to cook.
*Mama yetu anapika chakula sasa.*

**pikipiki** (pikipiki) a motor-cycle.
*Paulo ajua kuendesha pikipiki kama hii.*

**pili** the second one; the next one after the first.
*Nilimaliza somo la kwanza lakini sijaanza somo la pili.*

**pilipili** (pilipili) pepper.
*Chakula hiki kina pilipili nyingi.*

**pima** to measure; to examine.
*Pima urefu wa kamba hii.*
*Daktari alimpima mgonjwa.*

**pinduka** to be turned upside down; to be turned around.
*Motokaa ziligongana na moja ikapinduka.*

**pini** (pini) a pin.
*Nipe pini hiyo.*

**pini** (pini au mapini) a handle—such as the long wooden part of an axe.
*Shoka hili lina pini kubwa.*

**pipa** (mapipa) a barrel.
*Hili ni pipa la petroli.*

**pita** to pass something; to pass by something.
*Tutapita njia ile.*

**-po** is there; are there.
*Kalamu ipo hapa. Watoto wapo pale. Matunda yapo hapo.*

**poa** to be cool; to get cool.
*Chakula kimepoa sasa.*

**poa** to get well.
*Hamisi amepoa ugonjwa.*

**pokea** to receive.
*Nimepokea zawadi.*

**-pole** gentle or kind.
*Msichana huyu ni mpole.*
*Napenda watoto wapole kama hawa.*

**pole** never mind; words said because you are sorry for someone and want to make him feel better.
*Aliteleza, akaanguka matopeni, nami nikamwambia, 'Pole.'*
*Alipojiumiza nilimpa pole.*

**polepole** slowly.
*Kobe hutembea polepole.*

**polisi** (mapolisi) a policeman.
*Baba yake ni askari polisi.*

**pombe** (pombe) beer.
*Huyo hunywa pombe nyingi.*

**pona** to get well.
*Alikuwa mgonjwa lakini sasa amepona.*

**ponya** to make someone get well; to save someone.
*Daktari alimponya mgonjwa kwa dawa nzuri. Nilikuwa karibu kuzama maji lakini kaka yangu aliniponya.*

**popo** (popo au mapopo) a bat—that is, a little animal; like a mouse with wings, that flies at night.
*Nasikia sauti za mapopo.*

**pori** (mapori) a wild place having grass and bushes but not many trees.
*Amekwenda kuwinda wanyama wa porini.*

**posta** (posta) a post-office.
*Nenda posta ukanunue stampu.*

**potea** to be lost.
*Pesa zangu zimepotea!*

**poteza** to lose; to make something get lost.
*Kwa nini alipoteza mfuko wangu?*

**pua** (pua) a nose.
*Pua yako ni kubwa kuliko yangu.*

**pulizia** to blow on something or into something.
*Chakula changu kilikuwa cha moto, nikakipulizia kipoe.*

**pumzika** to have a rest.
*Kazi hii ni ngumu; tupumzike kidogo.*

**punda** (punda) a donkey.
*Punda kama huyu huweza kupeleka mzigo mzito.*

**punde** a little, especially a little time.
*Punde si punde nitamkuta rafiki yangu.*

**pungua** to decrease—that is, to grow smaller.
*Mvua inaanza kupungua.*
*Maumivu yangu yanapungua.*
**punguza** to make something get less or get smaller.
*Mwuzaji yule hataki kupunguza bei ya nguo anazoziuza.*
**pwani** (pwani) the shore of the sea or near the shore of the sea.
*Siku za likizo zikifika, watu wengi huenda pwani.*
**-pya** new.
*Gari hili ni jipya. Hadithi hii ina maneno mengi mapya.*
*Niletee kalamu mpya.*

# r

**raba** (raba) a rubber.
*Kazi ya raba ni kufuta alama za kalamu. Umeona raba yangu?*
**radi** (radi) a sudden sound of thunder.
*Sauti ya radi hutisha watoto.*
**rafiki** (rafiki au marafiki) a friend.
*Rafiki yangu ni mnene kidogo.*
**raha** (raha) comfort or rest.
*Baada ya kufanya kazi, kila mtu ataka raha.*
**rahisi** cheap; easy.
*Nguo hii si ghali; ni rahisi. Si rahisi kufaulu mtihani huo.*
*Nataka kununua mkeka rahisi.*
**raia** (raia) a citizen—that is, a subject of a country; someone who belongs to a certain country.
*Sisi ni raia wa Kenya.*
**rais** (rais au marais) a president—that is, someone who is the head of the government of a country which does not have a king.
*Rais wa Kenya ni mtu mwema.*
**ramani** (ramani) a map.
*Ramani hii ni ya Afrika.*
**rangi** (rangi) colour.
*Shati lake ni la rangi ya buluu.*
**rasmi** official; special, such as special clothes or a uniform which someone wears when he is working.
*Wanajeshi wamevaa nguo zao za rasmi.*
**redio** (redio) a radio.
*Umesikia redio yangu mpya?*
**-refu** long or tall.
*Wavulana hawa ni warefu.*
*Meza hii ni ndefu. Unataka ubao mrefu ama ubao mfupi?*
*Niletee kisu kirefu.*
**reli** (reli) a rail.
*Gari la moshi hupitia kwenye njia ya reli.*
**rifarii** (rifarii au marifarii) a referee—that is, someone who is a kind of judge of football games.
*Rifarii amepiga filimbi yake.*
**rinda** (marinda) a dress or skirt.
*Maria amevaa rinda jipya.*
**robo** (robo) a quarter of something; 15 minutes.
*Tulifika saa sita kasa robo.*
**roho** (roho) the soul—that is, something which makes you alive; it cannot be seen.
*Kila mtu ana roho yake.*
**rudi** to come back or return.
*Alikwenda Jumatatu akarudi Jumanne.*
**rudisha** to make something go back or come back; to give something back to someone.
*Kwa nini hujarudisha pesa ambazo nilikupa jana?*
**ruhusa** (ruhusa) permission—that is, being told that you can do something.
*Mwalimu alinipa ruhusa kuondoka katika chumba.*
**ruhusu** to tell someone that he can do something.
*Mama yetu alituruhusu twende.*
**ruka** to jump; to fly.
*Panzi aliruka mara nyingi.*

*Eropleni huruka angani.*

**rula** (rula) a ruler.
*Tafadhali, nipe rula yako.*

**rungu** (rungu au marungu) a big stick with a knob at the end.
*Mwivi alinipiga kwa rungu.*

**rusha** to make something jump; to make something fly.
*Je, unajua kurusha tiara?*

# S

**saa** (saa) an hour; a clock—that is, a little machine for telling time; a watch.
*Sasa ni saa tatu ya asubuhi.*
*Saa yangu imeharibika.*

**saba** seven.
*Nilipoteza shilingi saba. Mama alinunua viazi saba. Nitasoma somo la saba.*

**sababu** (sababu) a reason—that is, why something was done or is done.
*Sikununua baiskeli kwa sababu sikuwa na pesa. Mtoto alilia kwa sababu ya njaa.*

**sabini** seventy.
*Mzee yule ana umri wa miaka sabini. Nataka senti sabini na tano.*

**sabuni** (sabuni) soap.
*Miriamu alinawa mikono kwa kutumia maji na sabuni hiyo.*

**sadiki** to believe.
*Mimi nasadiki babari zake.*

**safari** (safari) a trip or journey.
*Niliporudi huku Paulo aliniuliza, 'Habari za safari yako?'*

**safi** clean.
*Kikombe hiki ni kichafu; niletee kikombe safi. Meza hii ni safi sana. Madirisha yote ni safi.*

**safiri** to travel.
*Tulisafiri kutoka Mombasa mpaka Kitale.*

**safisha** to make something clean.
*Nimesafisha meno yangu.*

**safu** (safu) a row or line.
*Mwalimu aliwapanga watoto katika safu tatu.*

**saga** to grind—that is, to rub something against something hard so that it is rubbed into little tiny pieces.
*Alisaga mahindi akapata unga wa mahindi.*

**sahani** (sahani) a plate or dish.
*Sahani yake kubwa ilitiwa chakula kingi.*

**sahau** to forget.
*Aliniambia jina lake, lakini nikalisahau.*

**saidia** to help.
*Mvulana huyo alinisaidia kutengeneza motokaa yangu. Nisaidie!*

**sakafu** (sakafu) the floor of a building or house.
*Sakafu ya nyumba hii ina uchafu mwingi.*

**salaam** greetings; a word said or written to greet someone.
*Sara alipomwandikia kaka yake barua, alianza hivi: 'Kaka mpenzi, Salaam nyingi sana.'*

**salama** fine; all right.
*'Watoto wako hawajambo?'*
*'Salama tu.'*

**sali** to say prayers.
*Ramadhani husali mara tano kila siku.*

**salia** to be left over.
*Watu wengi waliondoka; waliosalia walikuwa ni wachache tu.*

**salimu** to greet; to say hello to someone.
*Nilipomkuta rafiki yangu njiani nilimsalimu.*

**saluti** (saluti) a salute.
*Mgeni wa heshima alipokea saluti ya wanajeshi.*

**samaki** (samaki) a fish.

*Mto huu una samaki wengi sana.*

**samehe** to forgive.
*Nisamehe, mwalimu. Tulimkasirisha sana lakini baadaye akatusamehe.*

**sana** very; very much.
*Jitu ni mtu mkubwa sana. Unanisaidia sana.*

**sanaa** (sanaa) doing things well with your hands; a thing which someone has made with his hands.
*Anajifunza katika shule ya sanaa.*

**sanamu** (sanamu) a statue or doll.
*Sanamu hii ni ya mtu aliye mkuu.*

**sanduku** (sanduku au masanduku) a box.
*Sanduku hizi ni ndogo. Sanduku lile ni kubwa sana.*

**sarafu** (sarafu) a coin.
*Sarafu hii ni ya senti kumi.*

**sarafu**

**sarufi** (sarufi) grammar; the rules of language; putting the right words in the right order.
*Mazoezi haya yanahusu sarufi.*

**sasa** now.
*Usiende baadaye; nenda sasa.*

**sauti** (sauti) a sound; a voice.
*Mtoto mchanga alilia kwa sauti ya juu.*

**sawa** same.
*Jiwe hili ni sawa na hilo.*

**sawasawa** just the same.
*Damu huonekana sawasawa na rangi nyekundu.*

**sayansi** (sayansi) science.
*Mwalimu huyo ana elimu ya sayansi.*

**sayari** (sayari) a planet—that is, a small light which is seen in the sky at night and which is really another world going around our sun.
*Ile ni nyota na ile, inayong'aa zaidi, ni sayari.*

**sebule** (sebule) the first room which you come to as you enter a house through the front door; sometimes, a front verandah.
*Wazazi na watoto waliketi sebuleni, wakazungumza kwa muda wa nusu saa.*

**sehemu** (sehemu) a part or piece.
*Dreva huyo ajua kutunza sehemu za injini ya motokaa.*

**sekondari** (sekondari) secondary.
*Natumaini kuingia katika skuli ya sekondari.*

**sema** to speak or talk; to say something.
*Alisema kwa sauti ya juu. Mama alisema turudi saa tano.*

**semezana** to talk to each other about something.
*Wazazi wako wanasemezana.*

**sentensi** (sentensi) a sentence—that is, a word or group of words like any of the following words or groups of words which start with a big letter and end with a full stop or question mark:
*Ali amechoka. Amelala. Kitu hiki ni kikubwa. Maria yuko ubaoni. Yeye ndiye mwivi. Ana*

*kitabu. Anacho. Hayuko. Wewe mjinga. Yuko wapi? Alifanya nini?*

**senti** (senti) a cent.
*Senti hizi kumi ni zangu.*

**Septemba** (Septemba) September.
*Mwezi wa Septemba hufuata mwezi wa Agosti.*

**serikali** (serikali) government.
*Serikali ya nchi yetu ni nzuri sana.*

**shairi** (mashairi) poetry.
*Niliposikia shairi hilo nililipenda sana.*

**shaka** (shaka au mashaka) doubt—that is, being not sure of something.
*Bila shaka kutapambazuka.*

**shamba** (mashamba) a farm.
*Shamba lake ni kubwa.*

**shambuliwa** to be attacked.
*Vijiji vingi vilishambuliwa na mashifta.*

**shangaa** to be very surprised.
*Tulishangaa kuona ndege huyo hana mabawa yo yote.*

**shangazi** (shangazi) an aunt.
*Dada ya babangu ni shangazi yangu.*

**shangilia** to sing or shout because you are very happy about something.
*Siku ya Madaraka ilipofika tulishangilia sana.*

**sharti** (masharti) being necessary.
*Sharti tufanye tulivyoambiwa kufanya. Maneno yake si ya sharti.*

**shati** (mashati) a shirt.
*Mvulana amevaa shati jeupe na tai nyekundu.*

**shauri** (mashauri) plan.
*Naona ni shauri zuri twende pamoja.*

**shavu** (mashavu) a cheek—that is, the side of one's face.
*Shavu lake limevimba kwa sababu aliumwa na nyuki.*

**shawishi** to talk to someone nicely so that he does what you want him to do.
*Nilimshawishi, akakubali kufanya nilivyotaka.*

**sherehe** (sherehe) a big, happy ceremony.
*Mjumbe wa wilaya yetu alihudhuria sherehe ya kupanda miti.*

**sherehekea** to have a big, happy ceremony because of something.
*Wananchi wa Kenya husherehekea siku ya Kenya kujipatia uhuru.*

**sheria** (sheria) a law.
*Alishtakiwa kwa kuvunja sheria nyingi.*

**shetani** (mashetani) a devil or demon; something like a very bad fairy.
*Watu wa dini huchukia mashetani.*

**shiba** to be full of food.
*Siwezi kula zaidi; nimeshiba kabisa.*

**shida** (shida) trouble.
*Maskini huyo alipatwa na shida nyingi.*

**shika** to hold on to something.
*Kila mtoto alikuwa ameshika pesa zake mkononi.*

**shikamoo** hello.
*'Shikamoo mzee.' 'Marahaba mtoto.'*

**shikana** to hold on to each other.
*Watoto walishikana.*

**shilingi** (shilingi) a shilling.
*Hii ni noti ya shilingi hamsini.*

**shimo** (mashimo) a hole or pit.
*Hassan alianguka ndani ya shimo hili.*

**shinda** to win.
*Timu yetu ilishinda timu yao. Tumeshinda kabisa!*

**shinda** to spend your time; to pass the time away.
*Umeshindaje?*

**shindana** to try to win a game

against each other.
*Wachezaji wa timu zote mbili walishindana kiuma.*
**shingo** (shingo) a neck.
*Twiga ana shingo ndefu.*
**shirikiana** to work together and share with each other.
*Tushirikiane katika biashara hiyo.*
**shoka** (mashoka) an axe.
*Niletee shoka nikate mti huu.*

shoka

**shona** to sew.
*Rinda hili limepasuka; ni nani atakayelishona?*
**shtaka** (mashtaka) accusation; saying that someone else has done something wrong.
*Alishtakiwa lakini hakufahamu mashtaka yenyewe.*
**shtaki** to accuse; to say that someone has done something wrong.
*Nitamshtaki kwa kuiba pesa zangu.*
**shughuli** (shughuli) something which you do which keeps you busy.
*Siwezi kukusaidia sasa; nina shughuli nyingi.*
**shuhudia** to say that you saw something or that you know something is true.
*Nilishuhudia vitendo vyake.*
**shujaa** (mashujaa) someone brave; a hero.
*Tom Mboya alikuwa shujaa sana.*
**shuka** to come down.
*Safari ilikwisha, tukashuka kutoka katika gari la moshi.*
**shuka** (shuka) a piece of white cloth.
*Nitanunua shuka hii.*
**shukrani** (shukrani) thanks; thanking someone.
*Tulipokea shukrani zao.*
**shukuru** to say thank you.
*Alinisaidia, nikamshukuru sana.*
**shule** (shule) a school.
*Shule hii nzuri ina watoto mia mbili.*
**si** is not; are not.
*Huyu si mtoto. Vitu hivi si vibaya.*
**si-** this is indeed not; that is indeed not.
*Huyo siye Paulo. Hivyo sivyo vitu vyangu. Yale siyo matunda yake.*
**-si-** is not; are not; am not.
*Maskini ni mtu asiye na pesa. Hivi ni vitabu visivyo na picha. Umenunua shati lisilo na vifungo.*
**siafu** (siafu) safari ants—that is, brown insects which travel around together in a long line and which bite people and animals.
*Siafu wakija, nitawachoma kwa majivu ya moto.*
**siagi** (siagi) butter.
*Watoto watapaka mkate siagi.*
**sifu** to praise.
*Nilimsifu kwa tabia zake nzuri.*
**sigara** (sigara) a cigarette.
*Sigara kama hizi huharibu afya ya watu.*
**sihi** to ask or to beg.
*Maskini alimsihi tajiri.*
**sijambo** I'm fine, thank you.
*'Hujambo?' 'Sijambo.'*
**sikia** to hear; to feel.
*Tulisikia sauti yake. Nasikia njaa.*
**sikiliza** to listen.

*Sikiliza ninayoyasema!*

**sikio** (masikio) an ear.
*Punda huwa na masikio makubwa.*

**sikitika** to be sorry.
*Nimefanya makosa makubwa; nasikitika.*

**sikiza** to make someone hear something; to listen very carefully to something.
*Hakutaka kusikia maneno yangu lakini nilimsikiza.*
*Twataka Mungu asikize maombi yetu.*

**siku** (siku) a day.
*Nafikiri nitafanya kazi nyingi siku zijazo.*

**sikukuu** (sikukuu) a holiday.
*Hakutakuwa na skuli kesho kwa sababu ni sikukuu.*

**silaha** (silaha) a weapon—that is, something used to hurt or kill people or animals.
*Siku za zamani babu zetu walitumia silaha kama mikuki na mishale.*

**simama** to stand; to stop.
*Maskauti wote walisimama wima. Motokaa imesimama sasa.*

**simamisha** to make something stand or stop.
*Dereva alisimamisha lori.*

**simba** (simba) a lion.
*Simba wale wanakula nyati.*

**simile** move out of the way, please!
*Simile nipite!*

**simu** (simu) a telephone.
*Rafiki yangu alinipigia simu jana.*

**simulia** to tell a story; to tell a story to someone.
*Nyanya alitusimulia hadithi tamu.*

**sindano** (sindano) a needle.
*Nipe sindano hiyo na uzi huo.*

**sindikiza** to go part of the way with someone who is beginning a trip.
*Nilipokuwa nikianza safari yangu, kaka yangu alinisindikiza.*

**sinema** (sinema) a cinema—that is, a place where moving pictures are shown.
*Watoto hupenda kuona picha za sinema.*

**siri** (siri) a secret.
*Alifanya hivyo kwa siri.*
*Sitakuambia siri yangu.*

**sisi** we; us.
*Sisi tutakwenda peke yetu.*

**sisimizi** (sisimizi) an ant—that is, a small black insect.
*Sisimizi kama hawa hawaumi watu. Sisimizi hupenda kula sukari.*

**sita** to move very slowly because you do not want to go somewhere or because you do not want to do something.
*Ingawa mwalimu alimwita aliendelea kusita.*

**sita** six.
*Niletee viazi sita. Chupa sita zilivunjika. Umesoma somo la sita?*

**sitawi** to flourish—that is, to be in a very good way; to have nothing wrong.
*Twataka Afrika isitawi.*

**sitini** sixty.
*Nyanya ana umri wa miaka sitini. Baba ana shilingi sitini na tano.*

**siyo** no.
*'Yuko shambani?' 'Siyo. Yuko mjini.'*

**skauti** (maskauti) a scout—that is, a boy who has joined a special group of boys who go camping together and do other things like that.
*Skauti kama huyu huwa ni mwaminifu.*

**skuli** (skuli) a school.
*Sisi wanafunzi tunapenda skuli yetu.*

**soda** (soda) soda; a kind of

sweet drink, such as orange drink, which is sold in bottles.
*Mzazi aliwanunulia watoto wake soda chupa mbili.*

**sogea** to move closer to something or to move farther away from something.
*Sogea karibu kidogo, nataka kusema nawe.*

**soko** (masoko) a market.
*Soko la Nairobi ni kubwa sana.*

**soksi** (soksi) a sock.
*Soksi hizi ni chafu!*

skauti

**soma** to read.
*Unajua kusoma vitabu kama hivi?*

**somesha** to teach someone, especially to teach someone to read.
*Mwalimu anamsomesha mtoto.*

**somo** (masomo) a lesson.
*Masomo ya jana yalikuwa magumu.*

**songa** to press or press together; to stir or mix ugali until it is stiff.
*Ukisonga kitu hiki utakiharibu.*
*Mama anajua sana kusonga ugali.*

**songea** to move.
*Songea karibu kidogo.*

**staajabu** to be very surprised.
*Kuku alipotaga yai la dhahabu, tulistaajabu.*

**stahili** to be worthy of something.
*Rais wetu anastahili heshima.*

**stampu** (stampu) a stamp.
*Stampu hii ina thamani ya senti hamsini.*

**stesheni** (stesheni) a station.
*Stesheni ya gari la moshi huwa na wasafiri wengi.*

**sufuria** (sufuria) a sufuria; a kind of metal pot for cooking things in.
*Kuna maji ya moto ndani ya sufuria ile.*

**suka** to plait—that is, to twist something together, such as hair.
*Amesuka nywele zake vizuri.*

**sukari** (sukari) sugar.
*Tafadhali, tia sukari kidogo.*

**sukuma** to push.
*Tulimsaidia kwa kusukuma motokaa yake iliyoharibika.*

**sumbua** to bother someone.
*Mtoto huyo hunisumbua wakati wote.*

**sumu** (sumu) poison—that is, something which makes you

die if you eat it or if you get it inside of you.
*Nyati alipigwa na mshale wenye sumu, akafa mara moja.*

**sungura** (sungura) a hare—that is, an animal like a large rabbit; a rabbit.
*Sungura yule ana masikio marefu.*

**sura** (sura) appearance—that is, the way something looks.
*Msichana yule ana sura nzuri.*

**suruali** (suruali) trousers.
*Juma alipoanguka matopeni, suruali yake ilichafuka.*

**swala** (swala) an antelope or buck.
*Simba hupenda kula swala kama wale wakubwa.*

**swali** (maswali) a question.
*Maria hajafahamu swali lako, kwa hivyo hawezi kukujibu.*

**sweta** (sweta) a sweater; a jersey.
*Maria amevaa sweta yake mpya.*

# t

**taabu** (taabu) trouble.
*Maskini hupatwa na taabu nyingi.*

**tabia** (tabia) condition; being a certain way; the way something is.
*Huyu ni mtoto mwenye tabia nzuri.*

**tafadhali** please.
*Nisaidie, tafadhali.*

**tafuna** to chew.
*Babu hawezi kutafuna vizuri kwa sababu hana meno.*

**tafuta** to search; to look for something.
*Nimetafuta kitabu chako kila mahali lakini sijakipata bado.*

**tafutia** to look for something because of someone else; to help someone by searching for something.
*Tulimtafutia kitabu chake.*

**taga** to lay an egg.
*Kuku hutaga mayai.*

**tai** (tai) an eagle.
*Tai yule ni ndege mkubwa sana.*

**tai** (tai) a tie.
*Mwalimu amevaa koti na tai.*

**taifa** (mataifa) a nation or country.
*Taifa letu ndilo Kenya.*

**taja** to say something, especially to say the name of something or someone.
*Nilipotaja jina lake, akageuka.*

**tajiri** (matajiri) a rich person; someone who has a lot of money or a lot of valuable things.
*Tajiri yule mnene ana nyumba kubwa na motokaa mbili.*

**taka** to want; to need.
*Wafanyi kazi wanataka mishahara yao. Motokaa ile inataka kusafishwa.*

**takata** to be very clean and bright.
*Nimesafisha motokaa; sasa imetakata.*

**takataka** (takataka) rubbish; something without worth; something thrown away.
*Usitupe takataka sakafuni!*

**tamaa** (tamaa) desire—that is, wanting something very much.
*Tajiri huyo ana tamaa ya mali.*

**tamani** to want something very much.
*Mfungwa hutamani uhuru.*

**tambaa** to crawl or to creep.
*Mtoto mdogo anatambaa kwenda kwa mama yake.*

**tambua** to recognize.
*Nilipomkuta njiani sikumtambua.*

**tamka** to pronounce—that is, to say something in a certain way.
*Mgeni huyo hawezi kutamka jina langu.*

**tamu** (tamu) a term, a part of the school year, about twelve weeks long.
*Kila mwaka shuleni una tamu tatu.*

**-tamu** sweet.
*Sukari ni tamu. Maria alinipikia chakula kitamu. Maembe haya ni matamu.*

**tandaza** to spread something out.
*Tandaza nguo hizi juani.*

**tandika** to spread out something, like a blanket, over something else.
*Alitandika blanketi kitandani.*

**tandiko** (matandiko) something which is spread out over a bed, such as a blanket.
*Haya ni matandiko ya kitanda.*

**tandu** (tandu) a centipede—that is, a creature like an insect which has very many legs; it can bite.
*Usimkanyage tanda huyu.*

**tang'** the sound that a coin makes when it falls.
*Shilingi ilianguka tang'.*

**tanga** (matanga) a sail—that is, a big piece of cloth which is put up on a ship so that the wind will push the ship forward.
*Jahazi lile lina matanga makubwa.*

**tangaza** to proclaim or announce—that is, to make a lot of people know about something; for example, by saying something on the radio or putting it in the newspaper.
*Serikali ilitangaza kwamba ni lazima kila mtu alipe kodi.*

**tangazo** (matangazo) a notice or announcement—that is, something written or said to let a lot of people know some news.
*Je, unaweza kusoma tangazo lile?*

**tangu** since; from; from that time.
*Amekaa Uganda tangu kuzaliwa kwake. Sijamwona tangu siku hiyo.*

**tangulia** to go first.
*Juma alitangulia na Issa alikwenda nyuma yake.*

**-tano** five.
*Nina shilingi tano. Mkono una vidole vitano. Aling'oa magugu matano. Walisoma somo la tano.*

**tanua** to open something wide.
*Alitanua kinywa chake.*

**tapakaa** to be spread out all over the place and not in order.
*Nyota hutapakaa mbinguni. Vitabu vyako vimetapakaa deskini.*

**tapika** to vomit or throw up—that is, to be sick so that food you have eaten comes up again.
*Alikuwa mgonjwa, akatapika sana.*

**tapwi** the sound that something makes when it falls into mud.
*Niliteleza matopeni, nikaanguka tapwi.*

**taratibu** slowly and steadily.
*Mzazi aliwaambia watoto kula taratibu.*

**tarehe** (tarehe) date.
*Mgeni alifika tarehe gani?*

**tatizo** (matatizo) trouble; a difficulty—that is, something which makes something else hard to do.
*Kutokuwa na kazi ni tatizo kubwa.*

**-tatu** three.
*Wageni watatu wamefika. Naona miti mitatu. Nipe kalamu hizo tatu. Tutasoma somo la tatu.*

**taulo** (taulo) a towel.
*Baada ya kuoga, Juma alifuta mwili wake kwa taulo.*

**tawala** to rule a country or a place.

*Paka akiondoka, panya hutawala.*

**tawi** (matawi) a branch.
*Mti huu una matawi mengi makubwa.*

**tayari** ready.
*Hamisi yu tayari. Watu wote wako tayari.*

**tayarisha** to make something ready.
*Wafanyi kazi walitayarisha uwanja kabla ya mchezo wa mpira kuanza.*

**tazama** to look at.
*Tazama kitu kile!*

**tega** to trap something; to make a trap ready to trap something.
*Nilitega njiwa watatu.*
*Mwindaji anatega mtego.*

**tegemea** to depend on something else.
*Kila jengo lategemea msingi wake.*

**teka** to take water from somewhere.
*Msichana aliteka maji kisimani.*

**teke** (mateke) a kick.
*Mwalimu, huyu amenipiga teke!*

**tele** a lot of.
*Nilipewa pesa tele. Kule kuna maji tele. Huku kuna mchanga tele.*

**telemka** to go down or come down.
*Tulipanda mlima; halafu tukatelemka.*

**teleza** to make something fall or go down or slip; to slip.
*Sakafu hii inateleza. Mzee aliteleza matopeni, akaanguka.*

**tema** to cut something up.
*Mama anatema kuni.*

**tema** to spit—that is, to force out some of the stuff like water that is in your mouth.
*Usitome mate darasani!*

**tembea** to walk.
*Nilimwona akitembea kuelekea sinema.*

**tembelea** to go to visit someone; to walk around somewhere.
*Nataka kumtembelea ndugu yangu. Twapenda kutembelea pwani.*

**tembo** (tembo) an elephant.
*Karibu na Voi kuna tembo wengi.*

**tena** again.
*Usinipige tena. Hatukumwona tena.*

**tenda** to do something.
*Vitendo ulivyotenda ni vibaya sana!*

**tendo** (matendo) an action—that is something someone does, such as to move, to dance, to throw.
*Kumwokoa mtoto kulikuwa tendo zuri sana.*

**tenganisha** to keep some people away from each other.
*Watoto waligombana, nikawatenganisha.*

**tengeneza** to fix or repair.
*Mpira huu una pancha; Yohana atautengeneza mpira huu.*

**tetea** to speak for someone because you want to help him.
*Alipokuwa Ulaya, Jomo Kenyatta aliwatetea watu wa Kenya.*

**thamani** (thamani) the cost or worth of something; how valuable a thing is.
*Pete hii ina thamani kubwa.*

**thelathini** thirty.
*Ana umri wa miaka thelathini. Nahitaji shilingi thelathini na tano.*

**theluji** (theluji) snow.
*Juu ya mlima wa Kenya kuna theluji.*

**themanini** eighty.
*Ninahitaji senti themanini. Watu themanini walihudhuria mkutano.*

**thumuni** (thumuni) a fifty-cent

coin. *Nililipa thumuni tu.*

**tia** to put; to put in.
*Alitia maziwa katika chupa. Ninatia chai sukari.*

**tiara** (tiara) a kite.
*Kila mtoto hupenda kurusha tiara yake.*

tiara

**tifu** the sound that something makes when it falls into sand.
*Nazi ilianguka tifu.*

**tii** to obey; to do what someone tells you to do.
*Ni tabia njema kutii wazazi.*

**tikisa** to make something move one way and then move another way; to make something wave or shake.
*Alitikisa kichwa akasema, 'Hapana.'*

**tikisika** to wave or shake.
*Niliposukuma deski, kalamu zilianza kutikisika.*

**tilia** to put something in somewhere for someone.
*Tafadhali, nitilie chai sukari.*

**timia** to be finished.
*Nenda sasa; wakati umetimia.*

**timu** (timu) a team—that is, a group of people who play a game against another group of people.
*Timu yetu haishindiki.*

**tiririka** to move along like water.
*Machozi yalitiririka chini usoni mwake.*

**tisa** nine.
*Nililipa shilingi tisa. Watu tisa wanatukaribia. Sikusoma somo la tisa.*

**tisha** to frighten; to make someone afraid.
*Nyoka hutisha watu.*

**tisini** ninety.
*Nipe senti tisini. Alinunua stampu tisini na tatu.*

**tiwa** to be put in something or to be put somewhere.
*Viazi vimetiwa katika gunia.*

**toa** to take out something; to put out something; to take away something; to show something.
*Mwalimu alitoa kitabu chake. Ni lazima utoe makosa haya yote. Mimea inatoa maua mengi Nairobi.*

**toboa** to make a hole in something.
*Watu wa zamani walitoboa masikio yao.*

**tochi** (tochi) a torch—that is, a small lamp which someone can carry and which has batteries in it that make it work.
*Siwezi kuona vizuri; niletee tochi yako.*

**tofali** (matofali) a brick.
*Nyumba ile ilijengwa kwa matofali.*

**tofauti** (tofauti) difference; how something is different from something else.
*Kiti hiki ni sawa na hicho, lakini kile kina tofauti. Kuna tofauti baina ya hivi na hivyo.*

**togwa** (togwa) a kind of drink.
*Watoto hunywa togwa; watu wazima hunywa pombe.*

**toka** to come out or go out.
*Watoto wote wametoka darasani. Damu inamtoka Ali. Ali anatokwa na damu.*

**tona** to fall drop by drop.

*Nasikia maji yakitona.*

**tone** (matone) A drop.
*Maji yakitona, mimi nitahesabu matone.*

**toroka** to run away.
*Nilimrukia kondoo lakini akatoroka. Huyo alikuwa mfanyi kazi, akatoroka kazi yake.*

**tosha** to be enough.
*Pesa hizi zitatosha.*

**tota** to sink or drown.
*Kaka yake alitota maji mwaka uliopita.*

**tu** only; just.
*Tumefika sasa hivi tu. Hakuna mwingine; ni mimi tu.*

**tu** we are.
*Sisi tu tayari.*

**-tukufu** great; important.
*Rais wa nchi ni mtu mtukufu.*

**tukia** to happen; to happen to someone.
*Kulitukia nini? Jambo baya lilimtukia jana.*

**tulia** to calm down; to stop being excited; to be still.
*Kwanza mtoto alilia sana lakini baadaye akatulia, akalala usingizi.*

**tuliza** to calm someone down; to make someone stop being excited; to help someone be still.
*Mtoto alipolia mamake alimtuliza.*

**tuma** to send.
*Nitatuma mtu dukani kununua chumvi.*

**tumaini** to hope.
*Natumaini nitafaulu mtihani wa darasa la saba.*

**tumbaku** (tumbaku) tobacco—that is, the stuff in cigarettes.
*Alitia tumbaku kikoni.*

**tumbili** (tumbili) a kind of small monkey.
*Tumbili yuko mtini.*

**tumbo** (matumbo) stomach—that is, the part of the body in front from the waist up to the chest; the place where food goes when you swallow it.
*Tumbo lake ni kubwa kwa sababu yeye hula chakula kingi.*

**tumia** to use.
*Alikula kwa kutumia kisu na uma. Alitumia pesa zote bure.*

**tumikia** to serve.
*Askari polisi huwatumikia wananchi.*

**tunda** (matunda) fruit.
*Mti huu huzaa matunda mengi.*

**tundu** (matundu) a hole, especially a hole that an animal lives in.
*Bundi aliingia katika tundu lake.*

**tunga** to put in order.
*Tunga maneno haya yawe sentensi.*

**tunza** to keep something safe; to watch over something.
*Barua hii ina maana; uitunze.*

**tupa** to throw.
*Usitupe jiwe hilo!*

**tupia** to throw something at someone or to someone.
*Kwa nini ulinitupia mawe?*

**-tupu** empty.
*Alikwenda kwenye michezo ya farasi akarudi na mikono mitupu. Chombo hiki ni kitupu. Bilauri yangu ni tupu. Maneno yale ni uwongo mtupu.*

**tuta** (matuta) Soil that is piled up in a special way so that seeds or young plants can be planted in it.
*Mboga zilipandwa katika tuta refu.*

**twanga** to pound; to beat.
*Kutwanga ngano ni kazi ngumu. Timu yetu ilitwanga timu yao.*

**twiga** (twiga) a giraffe.
*Twiga huwa ni mnyama mrefu sana.*

# u

**u** you are; it is.
*Wewe, u tayari? Mkate u mtamu.*

**ua** to kill.
*Mwivi aliwaua watu wawili.*

**ua** (maua) a flower.
*Msichana alichuma ua zuri jekundu.*

**ua** (nyua) the back yard of a house; a fence or wall around the back yard of a house.
*Nyumba yetu ina ua mdogo tu. Nyua nyingi ni za makuti.*

**ubao** (mbao) a blackboard; a long, flat piece of wood.
*Ubao huu ni mweusi.*

**ubavu** (mbavu) a rib—that is, one of the bones in someone's chest.
*Mbavu zangu zaniuma tangu nilipoanguka.*

**ubawa** (mbawa) a wing.
*Ndege aliruka kwa kutumia mbawa zake.*

**ubaya** being bad.
*Simpendi kwa sababu ya ubaya wake.*

**ubwabwa** gruel—that is, a kind of rice soup that is not thick.
*Watoto wadogo hula ubwabwa.*

**uchafu** dirt.
*Deski yako ina uchafu mwingi!*

**uchaguzi** an election—that is, when people choose someone to be their leader.
*Mwaka wa sitini na tatu kulikuwa na uchaguzi mkuu nchini Kenya.*

**uchoyo** greediness; greed.
*Mtoto alionyesha uchoyo mwingi wakati alipochukua peremende zote na kuzificha chumbani mwake.*

**uchumi** the economy of a country: how many things are made each year in a country and how much money the country gets for selling these things.
*Twataka Kenya iwe na uchumi bora.*

**uchungu** a hurt which is very painful; being angry and bitter about something.
*Nilipopigwa sindano nilisikia uchungu. Alifutwa kazini akaonyesha uchungu mwingi.*

**udevu** (ndevu) a hair of a beard—that is, a hair that grows on someone's chin.
*Unamjua yule mwenye ndevu?*

**udongo** thick soil or clay.
*Kibanda hicho kilijengwa kwa miti na udongo.*

**udugu** being the brother, sister or cousin of someone else.
*Mimi humsaidia kaka yangu kwa sababu ya udugu.*

**ufagio** (fagio) a small broom or brush.
*Mama hawezi kufagia kwa ufagio huu kwa maana umeharibika.*

**ufito** (fito) a long, thin stick.
*Fito hizi ni ndefu sana.*

**ufuko** (fuko) the shore of the sea just above the water where there is lots of sand.
*Nilitembea ufukoni, nikaona kaa wengi.*

**ufunguo** (funguo) a key.
*Alifungua mlango kwa ufunguo wake.*

**ufunguo**



**ugali** a kind of food made from maize meal.
*Ugali huu ni mtamu.*

**ugeni** any country that is not someone's own country.
*Aliondoka katika Kenya,*

*akasafiri ugenini.*

**ugonjwa** (magonjwa) illness; being sick.
*Ugonjwa wake ulimsumbua sana.*

**ugua** to get sick; to feel bad.
*Mtoto analia kwa sababu ameugua.*

**uhai** life; being alive.
*Mdudu huyu amekufa; hana uhai.*

**uhuru** freedom; being free.
*Kenya ilijipatia uhuru mwaka wa sitini na tatu.*

**ujanja** a bad sort of cleverness; cunning.
*Katika hadithi za kiafrika sungura huwa anaonyesha ujanja mwingi.*

**ujenzi** (majenzi) building something.
*Anajua kujenga nyumba na sasa anatafuta kazi ya ujenzi.*

**uji** a kind of porridge usually made from rice, millet or maize meal.
*Walinipa uji, nikaunywa.*

**ujinga** being foolish.
*Walimcheka mjinga kwa sababu ya ujinga wake.*

**ujuzi** knowledge; having knowledge.
*Mzee huyu ana ujuzi mwingi.*

**ukali** fierceness; sharpness; bitterness; being fierce or sharp or bitter.
*Mbwa wake anaonyesha ukali kama wa simba. Nilisikia ukali wa kisu hicho. Dawa hii ina ukali mwingi.*

**ukanda** (kanda) a belt.
*Hamisi alinunua ukanda mpya.*

**ukarani** being a clerk.
*Mtu hawezi kufanya kazi ya ukarani bila kujua kusoma na kuandika.*

**ukili** (kili) A narrow strip of stuff made from a kind of leaf; it is used for weaving mats.
*Mamangu anajua kusuka ukili lakini mimi sijui.*

**ukindu** (kindu) a kind of leaf which is used for making baskets.
*Alikwenda msituni akakata ukindu mwingi kwa sababu alitaka kushona kikapu.*

**ukingo** (kingo) the edge of a river or a pit.
*Tulisimama ukingoni mwa mto.*

**ukoko** a hard crust—that is, stuff like the hard, dry rice that is found at the bottom and sides of the pot after wali has been cooked.
*Tunapenda kula wali lakini hatupendi kula ukoko wake.*

**ukoo** (koo) family.
*Mvulana huyu si kaka yangu lakini ni wa ukoo wangu.*

**ukosefu** lack; being without something.
*Watu wengine wanaotaka kufanya kazi hawawezi kwa maana ya ukosefu wa kazi nchini.*

**ukucha** (kucha) a claw or finger-nail or toe-nail.
*Simba ana kucha kali.*

**ukulima** farming.
*Kazi ya ukulima ni ngumu, lakini ina maana sana.*

**ukumbusho** something which makes people remember.
*Nairobi kuna jumba la ukumbusho,yaani muziamu.*

**ukunde** (kunde) a kind of bean.
*Napenda kula kunde kama hizi.*

**ukuni** (kuni) a stick of firewood.
*Nimeleta kuni nyingi.*

**ukurasa** (kurasa) a page—that is, one side of a piece of paper in a book or newspaper.
*Soma ukurasa wa pili.*

**ukuta** (kuta) a wall.
*Wamejenga ukuta mrefu.*

**ukwato** (kwato) a hoof; the foot

of an animal like a cow.
*Tulisikia sauti ya kwato za ng'ombe.*

**Ulaya** Europe; the land which is on the other side of the Mediterranean Sea; it has many different countries.
*Abud alikwenda Ulaya kusoma katika chuo kikuu.*

**ule** that one over there.
*Tazama mti ule. Nataka ufito ule.*

**ulimi** (ndimi) a tongue.
*Twiga huwa na ulimi mrefu.*

**ulimwengu** (malimwengu) the world.
*Ulimwengu huu una viumbe vya kila aina.*

**uliza** to ask; to question; to ask someone about something.
*Watoto huuliza maswali mengi. Nitamwuliza habari hiyo.*

**uma** to bite or to sting; to hurt.
*Nyuki walimwuma msichana. Kichwa chaniuma.*

**uma** (uma au nyuma) a fork—that is, something to eat with; it is like a metal comb at the end.
*Alikula kwa kutumia kisu na uma.*

uma

**umaskini** being poor.
*Hawawezi kununua cho chote kwa sababu ya umaskini.*

**umba** to make.
*Mungu aliumba ulimwengu.*

**umbali** distance; being far away.
*Kutoka Nairobi mpaka Nakuru ni umbali wa maili mia moja hivi.*

**umeme** lightning.
*Tuliona umeme angani, tukasikia radi; kisha mvua ikaanza kunyesha.*

**umia** to hurt; to be hurt.
*Jiwe lilimwangukia, akaumia vibaya.*

**umiza** to make someone hurt; to hurt someone.
*Aliniumiza kwa sababu alikuwa amekasirika.*

**umoja** unity or oneness; being one.
*Sisi sote, raia wa nchi hii yetu, tuwe na umoja kwa sababu umoja ni nguvu.*

**umri** age.
*Mtoto huyu ana umri wa miaka sita.*

**umuhimu** importance; being important.
*Kazi ya mwalimu ina umuhimu mwingi.*

**umwa** to be bitten or stung.
*Tuliumwa na nyuki. Niliumwa na mbwa.*

**unda** to build something, especially to build something out of wood.
*Yusuf anajua kuunda mashua.*

**unga** flour.
*Unga huu ni mweupe kabisa.*

**unga** to join.
*Unaweza kuunga hiki na hiki?*

**ungana** to join together.
*Tuungane mikono pamoja kazini.*

**unganisha** to join some things together.
*Unganisha vitu hivi viwili.*

**ungo** (maungo) a joint—that is, a place in your body where two bones are joined together; also, a part of the body.
*Nasikia maumivu maungoni.*

**ungua** to be burned; to get burned.
*Nyama yaungua!*

**unguza** to burn something or someone.

*Maji ya moto yaweza kumwunguza mtu.*

**unyasi** (nyasi) a leaf of grass.
*Ng'ombe hula nyasi nyingi kila siku.*

**unywele** (nywele) a hair.
*Nywele zangu si ndefu.*

**upakaji** putting colour on something by spreading it on with a brush.
*Yeye hufanya kazi ya upakaji wa rangi.*

**upande** (pande) a side.
*Angalieni karatasi hii; ina pande mbili, sivyo?*

**upepo** (pepo) a wind.
*Sikuweza kurusha tiara yangu kwa sababu hakukuwa na upepo wo wote.*

**upesi** quickly; fast.
*Nenda upesi!*

**upinde** (pinde) a bow.
*Mwindaji ana upinde na mishale.*

**upole** gentleness or kindness; being gentle or kind-hearted.
*Nampenda msichana huyu kwa sababu ya upole wake.*

**uraia** citizenship—that is, belonging to a certain country; being part of a certain country.
*Kila raia ajue maana ya uraia wake.*

**urefu** length or height; being so long or so tall.
*Mwalimu ana urefu wa mita mbili.*

**usafi** being clean.
*Nilichagua shati hili kwa sababu ya usafi wake.*

**usalama** peace.
*Tulinde usalama wa nchi yetu.*

**useremala** making things out of wood; being a carpenter.
*Baba yake hufanya kazi ya useremala.*

**ushanga** (shanga) a bead.
*Ni nani aliyekupa shanga hizi nzuri?*

**ushenzi** not knowing how to behave well at all.
*Mtu asiye na ustaarabu wo wote yuko katika hali ya ushenzi.*

**ushirika** working together.
*Makabila yote yalishirikiana, kukawa na ushirika mwema.*

**ushonaji** sewing.
*Yeye hutumia sindano na uzi katika kazi yake ya ushonaji.*

**usiku** (siku) night.
*Mgeni atafika usiku huu.*

**usiku wa manane** midnight.
*Watu huwa wamelala usiku wa manane.*

**usingizi** sleep.
*Watoto wote wamelala usingizi.*

**uskauti** scouting—that is, being one of the boys who has joined a special group of boys who go camping together and do other things like that; being a scout.
*Skauti huyo anapenda chama cha uskauti.*

**uso** (nyuso) face.
*Safisha uso wako!*

**ustaarabu** civilization; when everyone in a country knows how to behave well.
*Kitabu hiki chasema mengi juu ya ustaarabu wa Ulaya.*

**ustadi** knowing how to do something very well; being skilful.
*Sasa golikipa anaonyesha ustadi wake.*

**ustawi** growing in a good way; getting better and better.
*Twataka Kenya ipate ustawi.*

**uta** (nyuta) a bow.
*Mwindaji ana uta na mishale.*

**utajiri** having a lot of money or a lot of valuable things.
*Watu wanampenda huyo kwa sababu ya utajiri wake tu.*

**utumwa** being a slave; being

forced to serve someone else.
*Tunachukia biashara ya utumwa.*

**uuguzi** being a nurse; the work of helping sick people.
*Amina anataka kufanya kazi ya uuguzi.*

**uvivu** being lazy.
*Wazazi walikasirika kwa sababu ya uvivu wa mwanao.*

**uvumbuzi** discovering places; being an explorer.
*Salim anataka kufanya kazi ya uvumbuzi.*

**uwanja** (wanja) a flat place, especially a flat place in front of a house.
*Amina yuko uwanjani.*

**uwongo** a lie; something that is not the truth.
*Huyo amesema uwongo mtupu.*

**uyoga** (nyoga) a mushroom or toadstool—that is, a kind of little plant that is usually not green.
*Sitaki kula uyoga huu.*

**uza** to sell.
*Mwuzaji huuza vitu.*

**uzi** (nyuzi) thread or string.
*Uzi huu ni mwekundu.*

**uzuri** beauty; being beautiful.
*Kweli msichana yule ana uzuri mwingi.*

## V

**vaa** to put on clothes.
*Amevaa nguo mpya.*

**vazi** (mavazi) clothes.
*Askari wamevaa mavazi ya rasmi.*

**vema** well.
*'Umeshindaje?' 'Vema.'*

**vi** they are.
*Vitabu vi karibu nawe.*

**vibaya** in a bad way.
*Umefanya kazi yako vibaya.*

**vile** those ones over there.
*Niletee visu vile.*

**vile** in that way.
*Kwa nini alifanya vile? Paulo alichimba na Hamisi alichimba vile vile.*

**vimba** to swell; to get puffed up.
*Niliumwa na nyoka mguuni, na mara mguu ukaanza kuvimba.*

**vita** war; a battle or battles between two countries.
*Watu wengi walikufa katika vita vikuu.*

**vizuri** in a good way.
*Maria huimba vizuri sana.*

**vua** to take off clothes.
*Mtoto amevua nguo zake.*

**vua** to fish.
*Twendeni mtoni kuvua samaki.*

**vuja** to leak—that is, to let water out; to let water through.
*Paa la nyumba yake lavuja sana.*

**vuka** to go across.
*Daraja lilivunjika; hatukuweza kuvuka mto.*

**vuma** to roar or buzz or growl.
*Upepo unavuma nje ya nyumba.*

**vumbi** (mavumbi) dust.
*Vumbi liliniingia kooni, nikakohoa.*

**vumilia** to go on doing something or listening to something or watching something which you do not like at all.
*Siwezi kuvumilia makelele haya.*

**vuna** to harvest—that is, to gather together something, such as maize, which has grown on a farm.
*Afadhali tuvune shamba letu.*

**vunja** to break something.
*Usivunje chungu hicho!*

**vunjika** to be broken.
*Bilauri hii imevunjika; ni nani aliyeivunja?*

**vusha** to make someone or something go across.
*Tulipofika kwenye mto,*

*niliwavusha ng'ombe wote.*

**vuta** to pull.
*Mtoto anavuta gari lake. Uzuri wako ulinivuta hapa.*

**vutia** to be interesting.
*Hili ni jambo la kuvutia.*

# W

**wa** to be.
*Yeye hakuwa mgonjwa jana. Pesa zake zilikwisha, akawa mwivi.*

**wajibu** duty; what someone should do.
*Wajibu wa mtoto ni kumheshimu mzee.*

**waka** to burn.
*Moto umewaka vizuri.*

**wakati** (nyakati) time.
*Sikuweza kufanya kazi wakati huo.*

**wala** or.
*Sitaki soda wala pombe. Hana jembe wala shoka. Hajui kusoma wala kuandika.*

**wale** those ones over there.
*Unaweza kutambua watu wale?*

**wali** rice that has been cooked.
*Wali huu ni mtamu.*

**wao** they; them.
*Wao watakwenda peke yao.*

**wapi** where?
*Umeweka wapi kalamu yangu? Maria yuko wapi?*

**washa** to make something burn.
*Nitawasha moto sasa.*

**wasiwasi** doubt—that is, being not sure of something.
*Sijui kwa hakika; nina wasiwasi.*

**wavu** (nyavu) a net.
*Mpira uliingia katika wavu.*

**wayo** (nyayo) a mark on the ground made by a foot or hoof or paw.
*Tukifuata nyayo hizi tutapata swala.*

**wazi** open; easy to see or follow.
*Mlango wa darasa ni wazi. Njia hii ni wazi.*

**waziri** (mawaziri) a minister—that is, someone who is the head of a part of the government.
*Nilipokwenda kuona bunge, nilimwona Rais pamoja na mawaziri wake.*

**weka** to put; to put away.
*Mwalimu aliweka vitabu mezani.*

**wembe** (nyembe) a razor—that is, a kind of knife used for cutting off hair.
*Baba anatumia wembe wake.*

**weupe** whiteness; brightness; cleanliness; being white or bright or clean.
*Napenda ua hili kwa sababu ya weupe wake.*

**weusi** blackness; being black or dark coloured.
*Napenda jiwe hili kwa sababu ya weusi wake.*

**wewe** you.
*Wewe utakwenda peke yako.*

**weza** to be able to do something.
*Mzigo huu ni mzito; siwezi kuubeba. Huyu anaweza kufanya kazi nyingi.*

**wezekana** to be able to be done.
*Haiwezekani! Ikiwezekana, tutapanda mlima ule.*

**wika** to crow like a cock.
*Jogoo huwika asubuhi.*

**wiki** (wiki) a week.
*Mwaka huwa na wiki hamsini na mbili.*

**wilaya** (wilaya) a district.
*Nchini Kenya kuna wilaya nyingi.*

**-wili** two.
*Wasichana wawili wanaimba. Tunahitaji viti viwili. Alikula matunda mawili.*

**wima** being straight up and down.
*Maskauti wote walisimama wima.*

**wimbi** (mawimbi) a wave of water.
*Sikutaka kuingia katika mashua kwa sababu baharini kulikuwa na mawimbi mengi.*
**wimbo** (nyimbo) a song.
*Wimbo anaouimba ni mtamu.*
**winda** to hunt.
*Mwindaji huwinda kila siku. Ninawawinda swala.*
**wingi** plenty; lots of things or animals or people.
*Wageni hawakufika mmoja mmoja tu; walifika kwa wingi.*
**wingu** (mawingu) a cloud.
*Mawingu ya mvua ni meusi, manene.*
**wino** ink—that is, the coloured stuff, usually blue or black, that comes out of a pen when you write with it.
*Kalamu yako haina wino wa kutosha.*
**wizara** (wizara) a ministry—that is, a part of the government.
*Yeye anafanya kazi katika Wizara ya Elimu.*
**woga** fear; being afraid.
*Alipomwona simba, Maria alionyesha woga mwingi.*

# y

**ya** they are.
*Maua ya karibu nawe.*
**yaani** that is, in other words.
*Huyu ni mwashi, yaani mtu aakaye nyumba.*
**yadi** (yadi) a yard.
*Mkimbiaji yule hushinda katika mbio za yadi mia moja.*
**yai** (mayai) an egg.
*Mayai yote yalianguka, yakavunjika.*
**yale** those ones over there.
*Tazama majumba yale.*
**yaya** (yaya au mayaya) an ayah—that is, a woman whose work is to take care of someone else's child.
*Kule kuna mtoto na yaya wake.*
**yeye** he, him; she, her.
*Yeye atakwenda peke yake.*
**ye yote** anybody at all.
*Hakumsaidia mtu ye yote.*
**yowe** (mayowe) a scream; a sound which someone shouts.
*Alipomwona chui alipiga mayowe.*
**yu** he is; she is.
*Hamisi yu tayari.*
**yule** that one over there.
*Nenda kwa mvulana yule.*

# z

**zaa** to have a baby; to have fruit.
*Mwanamke amezaa mtoto. Mbuyu huzaa mabuyu.*
**zaidi** more.
*Pesa hizi hazitoshi; nataka zaidi. Alilala zaidi ya siku nzima.*
**zaliwa** to be born.
*Lizabet alizaliwa mwaka wa sitini na tatu.*
**zama** to sink or drown.
*Hakujua kuogelea, akazama majini.*
**zamani** a long time ago.
*Zamani sana kulikuwa na ziwa karibu na mlima wa Olorgesalie.*
**zawadi** (zawadi) a gift.
*Rafiki yangu alinipa zawadi mbili.*
**zeeka** to get old and be no good.
*Ndovu huyu amezeeka sana.*
**zeze** (zeze) a kind of banjo—that is, a thing with strings for making music.
*Anajua sana kupiga zeze.*
**zi** they are.
*Nyuzi zi karibu kukatika.*
**zidi** to grow bigger; to be more and more.
*Matata yamezidi nchini.*

*Wakulima wa Kenya wanazidi kupata faida.*

**zii** a painful tingling—that is, one sort of painful feeling which you may have in your teeth after eating something sour.
*Nilikula chungwa bichi na sasa meno yangu yanafanya zii.*

**zika** to bury—that is, to put a dead body in a hole in the ground.
*Walizika maiti jana.*

**zile** those ones over there.
*Deski zile zimevunjika.*

**zima** to put out a fire or a light.
*Nilizima moto kwa kuumwagia maji.*

**-zima** whole; not sick or hurt; grown up.
*Ukitaka maji, chukua chupa hii nzima. Sisi sote ni wazima. Ninyi ni watoto, si watu wazima. Amekula nanasi zima.*

**-zito** heavy.
*Kitu hiki ni kizito. Jiwe hili ni zito. Niletee mzigo ule mzito. Deski yako ni nzito sana.*

**ziwa** (maziwa) a lake.
*Ziwa la Naivasha lina samaki wengi.*

**zizi** (mazizi) a pen or enclosure or corral—that is, a place with a wall of sticks around it; animals are kept in it.
*Kuna ng'ombe wengi zizini.*

**zoa** to sweep up; to gather up something so that it can be taken away.
*Wasichana walizoa takataka zote.*

**zoea** to be used to doing something.
*Nilizoea kuamka kila asubuhi kabla hakujapambazuka.*

**zoezi** (mazoezi) an exercise.
*Mkimaliza zoezi hili, jaribuni mazoezi mengine.*

**zuia** to keep someone from doing something.
*Mwalimu alituzuia tusiondoke.*

**zuka** to appear suddenly.
*Panya alizuka kutoka ndani ya shimo.*

**zunguka** to go around and around.
*Gwaride lilizunguka uwanja mara mbili.*

**zungumza** to talk with someone.
*Tulizungumza kwa muda wa saa tatu.*

**-zuri** beautiful or good.
*Nionyeshe picha hiyo nzuri. Msichana huyu ni mzuri. Alinipa kitabu kizuri. Lile ni jengo zuri.*

**zurura** to wander around.
*Kwa nini unazurura huku mjini?*

**zzz** the sound that a bee makes when it flies.
*Nyuki alinikaribia zzz.*